SUPA JACKPOT
TZS. 1,117,417,539
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



MKONO WA POLE
**CRDB kutoa hadi mil.15/- mteja akifa**
UKURASA 3



UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Mei 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581321
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# Mapya yaibuka wakili aliyezua purukushani

• **Namba** ya uwakili anayotumia yadaiwa si yake... *Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO



UKURASA WA 3
### SABABU KUPOROMOKA LIFTI, KUJERUHI ZATAJWA
JESHI la Zimamoto na Uokoaji limesema...

UKURASA WA 4
### SERIKALI YAOMBA SIKU 14 KUMJIBU MKULIMA ALIYESHTAKI MAWAZIRI
SERIKALI imeomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, muda...

## Dk. Slaa aanika anavyoteta na Mbowe, Lissu
UKURASA 4



"Kuongeza shehena ya mzigo kutoka tani milioni 20.18 za sasa mpaka kufikia tani milioni 47.57 mwaka 2035. Kuongeza mapato yanayotokana na kodi ya forodha kutoka Sh. trilioni 7.756 mwaka 2022/23 mpaka kufikia Sh. trilioni 26.709 mwaka 2030. Tukifikia hapa asilimia 70 au 80 ya bajeti itatoka bandarini.

Mwonekano wa Bandari ya Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# Mbarawa ataja sifa nne mwekezaji Bandari ya Dar
UKURASA 2

MICHEZO MAGOLI 15 YALIVYOANDIKA HISTORIA YANGA UK.24 KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakizima moto uliokuwa ukiteketeza Kiwanda cha Jambo Plastic, Vingunguti jijini Dar es Salaam jana. Hakuna aliyejeruhiwa zaidi ya uharibifu mkubwa wa mali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mapya yaibuka wakili aliyezua purukushani

**Na Kulwa Mzee**

SAKATA la Wakili Baraka Mukama anayeshikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuzuia wateja wake kukamatwa, limechukua sura mpya baada ya mambo mengine kuibuka, ikiwamo namba ya uwakili anayodai yake, kusoma jina lingine.

Hayo yalibainika jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam ambako wakili huyo alitarajiwa kupandishwa kizimbani.

"Wakili yuko Kituo Kikuu cha Polisi anahojiwa. Mambo mengine yameibuka. Namba anayodai yake ya uwakili namba 4696, ukiingiza katika mfumo wa kujua mawakili, inasoma jina lingine la Nyando L. Nashon.

"Uchunguzi unaendelea katika suala hilo la namba na majina. Ukiwa tayari atafikishwa mahakamani wakati wowote," alisema Inspekta Sultani Mteta, Kiongozi wa Polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Vurugu hizo zilizoibuka juzi, zilitokana na uamuzi wa mahakama hiyo, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Romuli Mbuya, kuwaachia huru washtakiwa watatu waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka ya kughushi stika za dawa mbalimbali wakionyesha ni halisi wakati si kweli.

Hakimu Mbuya aliwaachia chini ya kifungu cha sheria namba 225 baada ya upande wa utetezi kupinga maombi ya Jamhuri ya kuahirisha shauri hilo.

Wakiwa mahakamani, Wakili wa Serikali, Faraji Nguka, aliifahamisha mahakama kwamba upande wa Jamhuri ulikuwa na shahidi mmoja lakini mtunza vielelezo ana udhuru, hivyo alishindwa kufika, hivyo wakaomba shauri lisikilizwe jana.

Wakili wa Utetezi Agatha Fabian, alipinga maombi ya Jamhuri, akaomba mahakama iliondoe shauri hilo mahakamani kwa sababu ni la muda mrefu.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja, ilikubali maombi ya wakili wa utetezi na kuwaachia huru washtakiwa chini ya kifungu namba 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Uamuzi huo wa Mahakama uliwafanya watuhumiwa Khalid Somole na Betty Mwankikusye kukimbia kwa lengo la kukwepa kukamatwa tena.

Washtakiwa wengine ambao hawakukimbia ni Raphael Lyimo na Abdiel Mshana.

Wakati watuhumiwa hao wakitaka kutoweka katika viunga vya mahakama, askari waliwazingira, wakitaka kuwakamata na ndipo wakili wao, Baraka Mkama, alipoingilia kutaka kuzuia hatua hiyo.

Walivutana kuanzia eneo la mapokezi hadi kwenye lango kuu la kutoka mahakamani. Wakili Mkama alifanikiwa kumsukuma askari Mbaraka Liyonjo getini.

Purukushani hizo zilimpa nafasi Betty kukimbia lakini askari walifanikiwa kumkamata Khalid pamoja na Wakili Mkama na kuwaweka mahabusu kwa muda kisha waliwapeleka Kituo Kikuu cha Polisi kwa hatua zaidi.

Katika kesi ya msingi washtakiwa wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la kughushi kati ya Machi Mosi na Machi 31 mwaka 2019.

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kuwa Machi 18, 2019, katika Mtaa wa Amani na Simba, Dar es Salaam, wakiwa na nia ovu, walighushi stika za dawa mbalimbali wakionyesha hazijapita muda wa kutumika na zimetolewa na Keko Pharmaceutical Industry (1997) LTD huku wakijua sio kweli.

# Mbarawa ataja sifa nne mwekezaji Bandari Dar

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amepigilia msumari hoja za wabunge kuhusu Bandari ya Dar es Salaam kuwa wanahitaji wawekezaji makini wenye sifa nne na ujuzi wa kimataifa.

Alizitaja kuwa ni kufikia viwango vya kimataifa na ufanisi utakaowezesha bandari kuwa shindani, uwezo wa kutoa ufumbuzi katika mnyororo mzima wa usafirishaji kutoka mzigo unaingizwa kwenye meli mpaka unafika kwa mteja.

Kuwa na mtandao mpana wa kupata mizigo kwenye soko la usafirishaji duniani, uwezo wa kimataifa wa kuendeleza na kuendesha shughuli za kibandari.

Alitaja sifa hizo juzi bungeni wakati akihitimisha hoja za wabunge waliochangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Mbarawa alisema, asilimia 37 takribani trilioni 7. 78 ya makusanyo ya mapato ya kiforodha ya TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) yanakusanywa Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema endapo watapata wawekezaji wenye sifa hizo, matokeo yake ni kupunguza muda wa meli kukaa kwenye nanga kutoka siku tano kwa sasa mpaka siku moja, na kuongeza idadi ya meli.

Alisema itapunguza muda wa ushushaji wa makasha kutoka siku nne za sasa mpaka siku moja na nusu, kupunguza muda wa uendeshaji mizigo kutoka saa mbili za sasa mpaka dakika 30.

"Kuongeza shehena ya mzigo kutoka tani milioni 20. 18 za sasa mpaka kufikia tani milioni 47.57 mwaka 2035. Kuongeza mapato yanayotokana na kodi ya forodha kutoka Sh. trilioni 7.756 mwaka 2022/23 mpaka kufikia Sh. trilioni 26.709 mwaka 2030. Tukifikia hapa asilimia 70 au 80 ya bajeti itatoka bandarini," alisema.

Pia, italinda ajira zilizopo na kuziongeza mpya mpaka kufikia 28,990, kushusha gharama ya usafirishaji na kuchangia kupunguza gharama za bidhaa zinazoingia na kuchagiza sekta zingine.

Alisema kumekuwa na utendaji usioridhisha wa bandari hiyo kwa mwaka 2015/16 ilihudumia mizigo tani milioni 15.67, mwaka 2022 takribani milioni 20.73 sawa na asilimia 30.5 likiwa ni ongezeko la asilimia 4.3, hata hivyo, alisema ni kidogo kutokana na mpango mkakati wa bandari ambao ni kati ya asilimia 10 mpaka 12.9 kwa mwaka.

Pia, alisema hakuna ufumbuzi mzima wa mnyonyoro wa usafirishaji wa mizigo kuanzia kwenye meli mpaka mdau na kwamba bandari hiyo ina ushindani mkubwa kwenye bandari nne duniani hasa kwenye mizigo ya Zambia, Malawi, Rwanda, Uganda na DRC.

"Bandari ya kwanza inayotupa presha na ushindani mkubwa ni Bandari ya Mombasa inamilikiwa na Mamlaka ya Bandari Kenya ina gati 17, magati 13 ni ya mizigo ya kawaida na sita ni kwa ajili ya kuhudumia makasha na kontena terminal II inahudumiwa na sekta binafsi. Bandari ya pili ni gati maalum kwa kushushia nafaka inaendeshwa na sekta binafsi

"Tusiogope sekta binafsi kuendesha bandari. Ni aibu mtu anasimama na kusema anaogopa sekta binafsi unaonekana mtu wa ajabu kwenye kuendesha bandari." Bandari nyingine ni ya Durban ina magati 50 na kati yake 31 ni ya kawaida na ya kuhudumia makasha ni 10 na magati kwa ajili ya mafuta makaa ya mawe na chuma yapo tisa yote yakiendeshwa na sekta binafsi.

"Bandari ya Berian, Msumbiji ina magari 11 ya shehena mchaganyiko na ya kushushia kontena inaendeshwa na sekta binafsi. Namibia gati ya kushushia makasha inaendeshwa na sekta binafsi. Bandari ya Morocco ina magati manne ya kushusha kontena na ina uwezo wa kushusha kontena milioni 9.9 kwa mwaka na zinaendeshwa na sekta binafsi, wakati ya Dar es Salaam inashusha kontena 760,000.

Alisema serikali ililazimika kuvunja mkataba wa TICS Desemba mwaka jana kwa kuwa haikuweza kuleta ufumbuzi katika mnyororo mzima wa usafirishaji wa mizigo na kushindwa kufikia viwango vya kimataifa vya ushushaji wa mizigo na matokeo yake meli zilikaa nangani kati ya siku 10 mpaka 14 na kulikuwa na ucheleweshaji wa utoaji mizigo bandarini.

Kuhusu hoja ya Bandari ya Bagamoyo, Mbarawa alisema endapo watahitaji meli kubwa yenye uwezo wa kubeba kontena 18,000 inayohitaji mita 250 ni lazima waende huko kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam ina mita 170, na katika mwaka huu wa fedha wanakwenda kuanza Bandari ya Bagamoyo.



HABARI KITAIFA

# Sababu kuporomoka kwa lifti na kujeruhi zatajwa

**Na Jenifer Gilla**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limesema chanzo kilichosababisha lifti kuporomoka katika jengo la Millennium Tower, Kinondoni mkoani Dar es Salaam na kujeruhi watu saba ni kukosa breki.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi hilo, Patrick Mohammed, lifti hiyo ilikosa breki kutokana na kuzidiwa na watu zaidi kuliko uwezo wake. Watu waliokuwamo wakati ajali hiyo inatokea walikuwa zaidi ya 10. Kwa kawaida lifti au chombo chochote kinachobeba watu kinakuwa na uzito maalumu.

Mohammed alisema licha ya kukosa breki, lifti hiyo pia ilikuwa katika matengenezo kwa muda wa wiki mbili mpaka tukio hilo linatokea, jambo linaloonyesha bado haikuwa na uwezo wa kubeba watu.

"Tunachoshauri hapa ni kuwa linapotekea jambo kama hili, wasianze kufanya majaribio kwa kupakia watu, bali vitu vyenye uzito unaolingana na watu na kutokana na hali hii sasa. Tunalazimika kufanya ukaguzi kwenye jengo zima," alisema.

Ofisa huyo alisema baada ya kufanya uokozi, waliwapeleka majeruhi katika hospitali ya Kairuki kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Tukio hilo lilitokea ikiwa ni siku moja baada ya kijana Joel Misesemo, maarufu MC Joe, mkazi wa Mwananyamala, kudaiwa kujiua kwa kujirusha kutoka ghorofa ya saba kwenye jengo la Derm Plaza lililoko karibu na Millennium Tower huku sababu za kuchukua uamuzi huo zikiwa hazijafahamika.

Meneja Masoko na Uhusiano wa Umma wa Hospitali ya Kairuki, Victoria Tarimo, alithibitisha kupokewa kwa majeruhi hao katika hospitali hiyo jana saa 5:00 asubuhi na kuwa wanaendelea na vipimo.

"Ni kweli tumewapokea na wanaendelea na vipimo kwa sasa, majibu yakishatoka ndio tutaweza kusema ni kwa kiasi gani wamejeruhiwa lakini kwa sasa wapo katika hali nzuri," alisema Tarimo.

**TAMKO PSSSF**

Kutokana na tukio la kuporomoka kwa lifti, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ambao ndio wamiliki wa jengo hilo, ulitoa pole kwa walioathirika na kuahidi kushughulikia hitilafu hiyo ili watumiaji waendelee na majukumu yao.

Taarifa iliyotolewa na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama wa Mfuko huo, James Mlowe, ilisema timu ya wataalamu wao kwa kushirikiana na msimamizi wa jengo hilo, wanaendelea na uchunguzi wa tatizo hilo na watatoa taarifa za kina hapo baadaye.

MKONO WA POLE

# CRDB kutoa hadi milioni 15/- mteja akifariki dunia

**Na Mwandishi Wetu,**

ARUSHA

JE, unajua kwamba Benki ya CRDB inatoa hadi Sh. milioni 15 pale mteja wake anapofariki dunia kama mkono wa pole? Unajua benki hiyo ina fungu lingine linalotolewa kwa mwenza aliyefiwa na mke au mume?

Benki ya CRDB imeanzisha utaratibu huo kwa wateja wake, ikitoa 'mkono wa pole' kulingana na aina ya akaunti ambayo mteja alifungua.

Katika Mkutano Mkuu wa 28 wa Mwaka wa Wanahisa wa Benki ya CRDB uliofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC), Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa Kati wa benki hiyo, Bonaventure Paul, alitoa ufafanuzi kuhusu bidhaa hiyo baada ya mmoja wa wanahisa kuomba kuwekwa utaratibu wa ndugu wa wanahisa kupewa mkono wa pole pale mwanahisa anapofariki dunia.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa tayari benki hiyo imeshaweka utaratibu wa kutoa mkono wa pole kwa wateja wake wote wenye akaunti zenye makato ya kila mwezi. Utaratibu huo ulianza rasmi mwaka 2021.

Alisema kuwa kwa akaunti ya akiba na akaunti ya mshahara, mteja akifariki dunia, katika akaunti yake benki itaweka Sh. milioni mbili. Kwenye akaunti ya mwenza wake benki inaweka pia Sh. milioni mbili.

"Kama aliyefariki alikuwa single (hajaoa au kuolewa), akaunti yake itawekewa Sh. milioni mbili. Kwa wateja ambao akaunti zao ni za Premier, kiasi chao ni Sh. milioni tano kama ikitokea kuna kifo.

'Kama alikuwa ameoa au kuolewa, maana yake Sh. milioni tano zitawekwa kwenye akaunti yake na Sh. miloni tano zingine zitawekwa kwenye akaunti ya mwenza wake.

"Kwa akaunti ya Tanzanite, hii tunatoa mkono wa pole wa hadi Sh. milioni 15, lakini vigezo ni vilevile. Akaunti hiyo uliyoifungua iwe na makato ya kila mwezi.

"Kwa akaunti hii mkono wa pole unaambatana na tiketi ya ndege ya kusafirisha mwili wa mteja wetu aliyefariki dunia. Pia tunatoa tiketi ya ndege ya msindikizaji," Paul alifafanua.

Akaunti ya Tanzanite ya Benki ya CRDB inahusisha watu walioko nje ya mipaka ya Tanzania. Hufunguliwa hata kwa fedha za kigeni.

Ili benki hiyo kutoa mkono wa pole, mwenza au ndugu wa mteja aliyefariki dunia wanapaswa kuwasilisha taarifa za kuthibitisha kifo, kikiwamo cheti cha kifo kilichothibitishwa kisheria.

Paul alisema maelezo zaidi ya bidhaa yao hiyo ya mkono wa pole yanapatikana katika matawi ya Benki ya CRDB yaliyotapakaa nchi nzima.

Katika ufuatiliaji wake, Nipashe imebaini kuwa kwa mwaka 2021, Benki ya CRDB ilitoa mkono wa pole Sh. bilioni 1.3 kwa wateja 601; mwaka jana (2022) ilitoa Sh. bilioni 2.1 kwa 1,028; na mwaka huu tayari imeshatoa Sh. milioni 664 kwa wateja 322.

Katika Mkutano Mkuu uliofanyika Jumamosi, wanahisa wa Benki ya CRDB waliidhinisha mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo kulipa gawio la Sh. 45 kwa kila hisa, hivyo kufanya jumla ya gawio kwa mwaka wa fedha 2022 kuwa Sh. bilioni 117.5.


# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| AGGREY | PAULO GIRIMBE RAWE | NYUMBA | PAULO GIRIMBE RAWE | KIVULE-ILALA | 29/05/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | SAMWEL JOHN GONZA | GARI-TOYOTA COASTER T966 DLX | SAMWEL JOHN GONZA | CCM MKOA-KILIMANJARO | 08/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | NEEMA SOLOMONI MWANGA | NYUMBA | NEEMA SOLOMONI MWANGA | BOMANG'OMBE | 09/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | MAIMUNA ABDALAH LEMA | NYUMBA | MAIMUNA ABDALAH LEMA | SHABAHA-MOSHI | 13/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | NOGRA ENTERPRISES CO.LTD | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI | NOEL FELIX NNKO | BOMANG'OMBE | 14/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HNP AND GENERAL SUPPLY LIMITED | NYUMBA | HELLY PETER NYONI | KIGAMBONI DEGE | 30/05/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | NORBERT LUDOVICK KWIYAKA | NYUMBA | NORBERT L.KWIYAKA | CHAMAZI DOVYA | 16/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | NYUMBA (2) | 1.HASSAN RAMADHANI HARASHI 2.HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | 1.YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE 2.TAMBANI MKURANGA | 16/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0715868000 /0754376493 /0714939933 /0759648448 /0759282344 /0753575752 /0655715138 /0787129539**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

MAZUNGUMZO

# Dk. Slaa: Ninapokutana na Mbowe, tunakumbatiana

• Anatumiana ujumbe na Lissu, wakosoana...

**Na Mwandishi Wetu**



Balozi mstaafu, Dk. Wilbroad Slaa, akifafanua jambo alipofanya mahojiano maalum na waandishi wa gazeti hili nyumbani kwake, Mbweni Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

ALIYEKUWA Balozi wa Tanzania Sweden, Dk. Wilbroad Slaa, amesema huwa anawasiliana na viongozi waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuhusiana na masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

Pia amekiri anafuatilia mikutano ya hadhara inayofanywa na chama hicho katika maeneo mbalimbali nchini kupitia kampeni mpya ya +255.

Dk. Slaa ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, amebainisha hayo katika mazungumzo maalum na waandishi wa Nipashe nyumbani kwake Mbweni mkoani Dar es Salaam.

Amesema huwa wanakutana katika mikutano ya mtandaoni (Club house). Pia huwa anawatumia ujumbe mfupi wa maandishi kwa simu ikiwa kuna jambo analotaka kushauri kwa viongozi hao.

Ameeleza kuwa hivi karibuni alimtumia ujumbe Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, baada ya kubaini amepotosha kuhusu taarifa ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), alipodai kuna ufisadi katika ujenzi huo. Amesema Lissu ameitumia isivyo ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika suala hilo.

"Lissu anasema reli ya SGR kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro imeandikwa kilomita kadhaa halafu CAG anasema zimepigwa kilomita 100. Sasa hapo kuna mambo mawili na bahati mbaya Lissu labda hana uzoefu wa ukaguzi.

"Mimi nimekuwa Mwenyekiti wa LAAC (Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa) na ninajua mkaguzi anakaguaje. Kwa hiyo, siongelei nadharia, ninaongelea hali halisi. Kumbuka reli ya SGR imeingia kwanza ndani, ikaenda mpaka maeneo ya Pugu huko halafu kuna kona nyingi, halafu inaingia Morogoro. Hilo pengo hapa katikati umelihesabia wapi?" amehoji.

Alisema katika mahesabu ya jumla ya mradi huo, CAG hajakagua, hivyo si sahihi kusema kuna wizi katika mradi. Dk. Slaa amesema hata CAG huwa anakosea ndiyo maana hotuba yake haijadiliwi bungeni hadi zihakikiwe na kamati za Bunge.

"Lakini sababu ya pili taratibu za reli nyingi duniani kuna laini ya kwanza, kuna laini ya pili na kuna laini ya tatu. Kwa hiyo, kuna mahali mnafika mnataka kukutana inachepushwa, inahamishwa ili ziweze kupishana, hizi hazijahesabiwa" ameeleza.

Dk. Slaa pia amesema anaamini CHADEMA ndicho chama pekee chenye ushawishi kwa wananchi kati ya vyama vyote vya upinzani nchini, hata kufikia hatua ya kupewa uongozi wa nchi.

Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo ya Dk. Slaa na waandishi wa Nipashe:-

***SWALI: Unawasiliana na viongozi wa CHADEMA?***

***DK. SLAA:*** Kwanini unauliza hivyo? Kuna njia nyingi za kuwasiliana. Kama hapa nimewaambia nilikuwa ninafuatilia mkutano wao lakini ushauri wanapewa na vyombo vyao vya kikatiba. Mimi sipo katika hivyo vyombo. Ninawasiliana nao kwa njia ya kufuatilia nini kinaendelea na kama siridhiki siku hizi kuna njia nyingi, ikiwamo club house mtandaoni. Kama unaingia huko utanisikia.

Nikikutana na Mbowe, mara nyingi kwenye pilika mbalimbali, tunakumbatiana! Sasa zaidi ya hapo tuwasiliane nini?

***SWALI: Ni upi mtazamo wako kuhusu kampeni mpya ya CHADEMA ya +255 Katiba Mpya?***

***DK. SLAA:*** Moja ambalo nimeliona kupitia mikutano hiyo ni kuwa wananchi walikuwa na kiu na kwa hiyo mahudhurio ni makubwa sana. Mwitikio ni mkubwa sana.

La pili ni uelewa wa wananchi . Wana uelewa sana tofauti na tulipotoka kule nyuma. Na hii ni kutokana na hali ilivyokuwa miaka mitano iliyopita. Operesheni hiyo ya CHADEMA ninadhani inataka kuwarudisha wananchi kwenye mstari. Kuna mkazo mkubwa wa wananchi kutaka ukombozi.

***SWALI: Ulionekana kwenye jukwaa la CHADEMA hivi karibuni. Je, ni maandalizi ya kurejea katika siasa?***

***DK. SLAA:*** Ninashukuru umeuliza hili. Kwanza kabisa, mtambue ya kwamba Karatu ni nyumbani kwangu na mimi ni mzee sawa na wazee wa Karatu. Kwa hiyo, panapokuwa na tatizo, mimi siwezi kujitenga. Siku hiyo nilikuwa ninazungumza kama mtu wa Karatu.

Yaliyotokea mwaka 2020 yalivuruga kila kitu katika mfumo wa siasa ya nchi na sasa niliokuwa ninawalalamikia ndiyo walioharibu. Kilichotokea ni kwamba waziri alikwenda Karatu, akauvuruga mradi wa maji wa wananchi ulioanzishwa miaka 23 iliyopita na bahati nzuri mimi nilikuwa mwanzilishi wa mradi huo nikiwa Mbunge wa Karatu.

Tukausajili kwa sheria za nchi na hata siku moja wananchi hawakukosa maji. Mradi ulifika kilomita 500 za bomba. Sijui kama mnaelewa kilomita za bomba ila ni kama umbali wa Moshi kuja Dar es Salaam.

Ameingia waziri, amevuruga menejimenti ya bodi ya maji na kuiunganisha na bodi ya serikari kinyume cha sheria na sasa wananchi kwa miezi karibu 10 hawakuwa na maji.

Unategemea mimi ambaye nilianzisha mradi huo, ninajua historia ya mradi, ninajua sheria yake na nilisimamia bungeni, halafu waziri anaamka anakwenda kutoa tamko. Ni watu waliolewa madaraka, wasioelewa kuwa taifa linahudumiwa na kila mtu mwenye uwezo wa kuchangia.

Kwa hiyo, nilipaswa kwenda Karatu na kukemea ile hali, lakini nisingeweza kukemea kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho waziri wake aliharibu. Ingekuwa maajabu.

Ilikuwa dhahiri kuwa njia ya kuongelea ni kupitia CHADEMA, lakini lazima ujue Karatu CHADEMA, hata kama mwaka 2020 walinyang'anywa. Ndiyo chama tawala kwa Karatu mpaka kesho kwa sababu chama kiko kwenye mioyo ya watu.

***SWALI: Umesikika ukitamka CHADEMA imekomaa. Una maana gani?***

***DK. SLAA:*** Ni sahihi. Mimi nilizungumzia kwa muktadha wa Karatu kwamba kwa kutazama kile kilichokuwapo Karatu, CHADEMA ndiyo chama tawala, lakini unaweza kuangalia nchi nzima. Kwa hali ilivyo, nimeona kutoka Morogoro mpaka kuingia Kigoma juzi. Ukifuatilia, CHADEMA imekomaa.

Imekomaa kwa sababu CCM inatumia madaraka ya dola sio mapenzi ya wananchi. Katika nchi ya kidemokrasia hatutegemei polisi, chama tawala kiongoze kwa kuwa polisi wapo pale, wanatisha wananchi au waende wanyang'anye masanduku ya kura.

Nilitegemea mama (Rais Samia Suluhu Hassan) ambaye anajitambulisha kama mtu wa demokrasia, haya mambo yatoweke. Lakini kilichotokea Karatu, miradi ya wananchi inakufa. Ni tatizo la chama kimoja kulewa madaraka, ndiyo maana uliona juzi wafanyabiashara (Kariakoo) walipiga kelele kwa sababu haki zao ziliingiliwa.

****USIKOSE KUFUATILIA KESHO MSUGUANO WAKE NA MWALIMU JULIUS NYERERE***

## Serikali yaomba siku 14 kumjibu Mkulima aliyewashtaki mawaziri

**Na Grace Gurisha**

SERIKALI imeomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, muda wa siku 14 kuwasilisha kiapo kinzani katika maombi yaliyofunguliwa na Thomas Nkola, maarufu kama Mkulima, ya kutaka kuwafungulia mashtaka vigogo wa serikali.

Vigogo hao ni Waziri wa Fedha, Dk Mwigulu Nchemba, Profesa Makame Mbarawa (Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi), mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Mkosa Jinai, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP).

Maombi hayo namba 16 ya mwaka 2023 yaliwasilishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Evodia Kyaruzi, kwa ajili ya kutajwa. Upande wa serikali ulidai kuna baadhi ya nyaraka hujazipata (hati ya wito), hivyo kuomba siku 14 kwa ajili ya kuwasilisha kiapo hicho.

Wakili wa Mkulima, Penina Ernest, alitoa hati mbili na kuukabidhi upande huo na kudai kuwa zingine atazipeleka ofisini. Hakimu Kyaruzi aliahirisha maombi hayo hadi Juni 6, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa na kuangalia kama kiapo hicho kimewasilishwa mahakamani hapo.

Katika hati ya maombi hiyo, Mkulima anadai kuwa kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) wakati akitekeleza majukumu yake, Dk Nchemba, Prof. Mbarawa na Mativila katika mwaka wa fedha 2021/22, walisababishia serikali hasara ya Sh. 2,914,113,070,000 licha ya kupangiwa bajeti ya ujenzi wa barabara ambayo ni asilimia 99 ya kiasi kilichobaki ambacho kingetekelezwa kwa jumla na kwamba fedha hizo hazijulikani.

Mkulima anadai kuwa pamoja na tuhuma zote zilizoibuliwa na CAG katika ripoti yake ya mwaka 2021/22 kuonyesha hasara kubwa iliyoipata serikali ya Tanzania, walalamikiwa kuwa wanahusika huku Mkurugenzi wa Upelelezi wa makosa ya Jinai na Ofisi ya DPP zikiwa hazijachukua hatua zozote za kisheria dhidi ya viongozi hao kwa kuwahoji.

Pia hati hiyo inaeleza kuwa hata Bunge baada ya kupokea ripoti za CAG, Spika wa Bunge hajalitilia maanani kwa kuwa Bunge limepanga kujadili ripoti hiyo Novemba, mwaka huu hali ambayo jambo hilo litakuwa limepitwa na wakati na watu hao watakuwa wamepokea fedha zingine katika bajeti ya mwaka 2023/24 kwa mradi huo huo.




Meneja Mkuu Raslimali Watu wa Tembo Nickel, Simon Sanga, akizungumza na wahitimu wa chuo waliochaguliwa kwenye 'Tembo Nickel Young Talent Graduate Program' mwaka huu, wilayani Ngara mkoani Kagera hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tembo Nickel yavutia vijana 7,000 fursa ajira

**Na Mwandishi Wetu,**

NGARA

KAMPUNI ya Tembo Nickel imeanza utekelezaji wa programu maalum ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa fani mbalimbali za elimu ya juu inayojulikana kama 'Tembo Nickel Young Talent Graduate Program'.

Kwa awamu ya kwanza, wahitimu 10 wameanza mfunzo ya mwaka mmoja wakiwa ni miongoni mwa zaidi ya 7,000 walioomba kujiunga na programu hiyo.

Meneja Mkuu wa Rasilimali Watu wa Tembo Nickel, Saimon Sanga, akizungumza baada ya kupokea wahitimu hao katika eneo la mradi wa Kabanga Nickel wilayani Ngara mkoani Kagera, alisema mafunzo hayo kwa vitendo kwa mwaka mmoja ni endelevu.

Alisema yanalenga kutoa fursa ya ujuzi kwa vijana wa kitanzania kutoka kwa wataalamu wabobezi wa ndani ya nchi na wa nje ya nchi wanaofanya kazi katika mradi huo wa kitaifa.

"Tumeanza kwa kuchukua vijana 10 wenye taaluma tofauti. Kwa kuwa mpango huu ni wa kila mwaka, tutakuwa na vijana wengine kwa mwaka 2024/25, na idadi itaendelea kuongezeka kutokana na ukuaji wa mradi wenyewe.

"Jambo lingine la msingi ni kwamba ukiwaambia watu kwamba walioomba ni zaidi ya 7,000, watu wanaogopa. Tusichukulie hiyo kama changamoto, tuichukulie kama fursa. Hawa vijana 7,000 ambao wote wana digrii, ni tunu kwa taifa.

"Endapo kampuni zingine zikiendelea kuwachukua na kuwapa mafunzo, baada ya miaka michache ijayo tutakuwa hatuna haja ya kwenda mbali kutafuta ujuzi. Tutakuwa na watu wengi wenye ujuzi katika taifa letu," alisema Sanga.

Kuhusu uwiano wa kijinsia, Sanga alisema kati ya vijana wote walioingia katika mpango huo, 50 ni wanamume na 50 ni wanawake.

"Suala la jinsia kwetu Tembo Nickel ni jambo tunalolichukua kwa umakini mkubwa. Ukiangalia hata kwa takwimu pale ofisi ya Dar es Salaam, idadi ya wanawake ni asilimia 67 na wanamume ni 33. Tunataka kuona hilo linatokea katika mradi hapa Ngara," alisema.

Kuhusu maeneo walipotoka wahitimu hao, Sanga alisema ni sera ya Tembo Nickel kutoa vipaumbele kwa wakazi wa Ngara, hivyo asilimia 50 ya wahitimu waliojiunga na mpango huo wanatoka Wilaya ya Ngara na waliobaki wanatoka katika wilaya zingine za Mkoa wa Kagera.

"Tulichukua idadi ya watu wote ambao waliomba, tukaanza kuangalia vigezo. Kwa sababu tunajua wengine wanomba tu kwa sababu kuna fursa hata kama hawana vigezo. Kwa hiyo, kwanza tuliangalia vigezo kisha tukaweka kwenye mafungu mawili, kundi la kwanza ilikuwa ni wale ambao wanatoka Wilaya ya Ngara ili kuhakikisha wakati tunafanya usahili kunakuwa na uwiano wa kutosha," alisema

Noela Msimangilo, mhitimu wa fani ya rasilimali watu (HR), alisema alipata taarifa ya mpango huo kupitia kundi la mtandao wa WhatsApp la wanafunzi waliohitimu pamoja.

"Ninaamini hapa nitapata mafunzo mazuri, tumepokewa vizuri, tunafundishwa vizuri sana. Ninategemea ujuzi wangu utakua sana na ninatarajia kupata uzoefu mkubwa na kuja kuwa Meneja wa Raslimali Watu mkubwa. Ninaamini nimefika eneo sahihi. Nishauri tu vijana wenzangu wakiona matangazo ya kazi waombe, wasijiulize sana," alisema.

Paul Mgisha, mnufaika wa mpango huo aliyesomea masuala ya fedha, alisema aliona tangazo hilo katika mtandao wa Twitter na kuamua kuomba nafasi hizo.

"Mchakato wote wa usahili ulikuwa wa wazi. Tulifanya usaili katika hatua mbalimbali na baada ya hapo nilipigiwa simu kutakiwa kujiandaa kuja kwenye mradi," alisema.

# Kampuni 20 China zaonyesha nia kuwekeza Tanzania

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI 20 kutoka mji wa Foshan nchini China, zimeonyesha nia ya kuwekeza katika sekta mbalimbali Tanzania ikiwamo ujenzi wa kiwanda cha madini.

Uamuzi wa kampuni hizo kuwekeza Tanzania, umetokana na kile kilichoelezwa na wawakilishi wao kuwa wamevutiwa na mifumo na mazingira ya biashara nchini.

Kampuni hizo zimewasili nchini juzi kutoka Foshan, katika Jimbo la Guangdong, China kuangalia mazingira ya kuwekeza.

Akizungumza katika mkutano na wadau wa uwekezaji na biashara wa Tanzania, mmoja wa wawakilishi wa wawekezaji hao, Yang Wu, alisema uamuzi wa sekta watakazowekeza utatokana na mazungumzo na wafanyabiashara wa hapa nchini.

"Tunatarajia kufanya mazungumzo na watu kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na baada ya kutueleza mifumo ya biashara ya hapa, ndipo tutaamua tunafanya biashara gani," alisema.

Lakini kwa sasa, alisema wanatarajia kuanzisha kiwanda cha kuchakata madini na maeneo ya biashara.

Kwa mujibu wa Wu, wataendelea kukutana na wadau mbalimbali wa biashara na uwekezaji nchini kwa ajili ya mazungumzo kuona maeneo yepi yenye fursa zaidi.

Meneja wa Fedha wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Deogratius Massawe, alisema jukumu lao ni kuhakikisha wanawaunganisha wadau na wawekezaji hao.

"Tutaendelea na mazungumzo nao, tukiamini nafasi mbalimbali za biashara na fursa zitapatikana kufuatia mkutano huu," alisema.

Pamoja na wadau hao kuwasili Tanzania, Massawe alisema TPSF inatarajia kuratibu safari ya wafanyabiashara wa Tanzania kwenda Foshan itakayofanyika mwaka huu.

Hamasa na fursa za uwekezaji nchini ni miongoni mwa taarifa walizopewa wawekezaji hao, imeelezwa na Dayana Lumanga, Ofisa Uhamasisha Uwekezaji wa TIC.

"Tunachohitaji ni kuwahamasisha kuhusu maeneo wanayopaswa kuwekeza na fursa zilizopo na tunawakaribisha ofisini kwa mazungumzo zaidi na hapa tumewaeleza kuhusu fursa zilizopo kwenye uwekezaji katika sekta ya kilimo," alisema.

James Maziku ni Mhamasishaji wa Uwekezaji kutoka EPZA, ambaye alisema wanayo maeneo kadhaa ya uwekezaji kwa ajili ya wafanyabiashara kutoka mataifa mbalimbali.

"Sisi tunaweka kabisa miundombinu na kwenye wasilisho letu tumewaeleza kuhusu mradi wa uwekezaji wa Bagamoyo," alisema.

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD**
**P.O.BOX 12943**
**ARUSHA**

**NOTISI/ MARUDIO YA TANGAZO LA MNADA**

Kwaidhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK,** tunatoa muda wa siku saba (7) kwa mdaiwa aliyeorodheshwa kwenye jedwali hapo chini ili aweze kulipa deni analodaiwa kwa muda mrefu, kama hatafanya hivyo dhamana yake kama ilivyoorodheshwa kwenye jedwali itauzwa kwa mnada wa hadhara.

| JINA LA MDAIWA | KINACHOUZWA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE |
|---|---|---|---|
| EMMANUEL ANAEL OWISO | NYUMBA | NYUMBA ILIYOPO MTAA WA TEGETA "A" KATA YA GOBA MANISPAA YA UBUNGO MKOA WA DAR ES SALAAM | 02/06/2023 NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atakayeshinda atapaswa kulipa kiasi cha asilimia 25%au zaidi ya bei itayofikiwa mara baada ya nyundo ya dalali kuanguka na fedha inayobaki itapaswa kulipwa ndani ya siku 14 kuanzia siku ya mnada na endapo mnunuzi akishindwa kulipwa fedha ilibaki basi fedha ya awali iliyopo haitarudishwa na mnada utarudiwa

2. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo.

3. Gharama za kubadilisha hati ya umiliki ni za mnunuzi mwaenywe.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA SIMU NO; 0752632033 AU 0628512033**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mahakama ijitathmini kiutendaji watendaji kujihusisha na rushwa

**MHIMILI** wa Mahakama mara kwa mara umekuwa ukitajwa kuwa miongoni mwa taasisi zinazoongoza kwa tuhuma za rushwa kutokana na baadhi ya watendaji kuhusishwa na vitendo hivyo na hatimaye kupindisha haki.

Kila Taasisi ya Kuzuia na Kudhibiti Rushwa (TAKUKURU) inapotoa taarifa kuhusu hali ya rushwa, Mahakama imekuwa moja ya taasisi zinazotajwa kuwa vitendo vya rushwa vimekithiri.

Kutokana na tuhuma hizo, kama msemo maarufu wa 'Rushwa ni Adui wa Haki' usemavyo, kushamiri kwa vitendo hivyo kumesababisha watu wanaostahili kukosa haki kwa sababu kinachoangaliwa si nani mwenye haki bali mwenye dau kubwa analopenyeza kwa mahakimu au kwa majaji. Kwa maneno mengine, mwenye donge nono ndiye anayeshinda shauri likifikishwa mahakamani badala ya mwenye haki.

Mathalan, katika mashauri mbalimbali yanayohusu migogoro ya wakulima na wafugaji, kumekuwa na taarifa kuwa kutokana na wafugaji kuwa na fedha, ndio wamekuwa wakishinda kesi nyingi hata kama wakulima wana haki. Hali hiyo inasadifu na kauli aliyowahi kuitoa mwanasheria nguli nchini, Jaji Joseph Warioba, kuwa: "Kutokana na Mahakama kulalamikiwa kuwa ni miongoni mwa taasisi zinazohusishwa kwa rushwa, watu wamefikia hatua kusema mahakamani kuna sheria lakini hakuna haki."

Kauli hiyo ya Jaji Warioba aliyoitoa mwaka 1996 bado inaishi mpaka sasa kutokana na mhimili huo kuelezwa kuwa bado umejaa harufu ya rushwa, hatua ambayo inafanya jamii kukosa imani nao.

Juzi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakati akiwaapisha majaji wapya wa Mahakama ya Rufani Tanzania, alirejea kauli hiyo ambayo imeishi miaka mingi kwamba mhimili huo unapaswa kujitazama upya kuhusu utendaji wake katika kutoa haki kutokana na manung'uniko ya wananchi kwamba umenyoshewa kidole kuhusu rushwa. Bila kuuma maneno, Rais aligongelea nyundo msumari kuhusu rushwa kukithiri katika kesi za wafugaji, hivyo kukwamisha utoaji wa haki.

Rais alitoa mfano wa kesi ya wafugaji mkoani Lindi ambayo iliibua ukakasi juu ya mwenendo wake baada ya wafugaji kukamatwa kuwa wamefanya makosa lakini jaji mmoja akasema hawajafanya. Kutokana na ukakasi huo, Rais alisema inaonyesha dhahiri kwamba wafugaji wamekuwa wakitembeza rupia kwenye udhia kwa lengo la kushinda kesi kwa namna yoyote ile.


Kuwapo kwa mambo kama hayo, Rais aliagiza Baraza la Maadili kuvalia njuga malalamiko hayo kwa kuwachunguza majaji na mahakimu, huku jicho likiangazia zaidi watendaji wa ngazi za chini kuanzia mahakama za mahakimu wakazi za mikoa, wilaya na zile za mwanzo ambazo zinatajwa kuwa mstari wa mbele katika kujihusisha na vitendo hivyo vinavyokwamisha upatikanaji wa haki.

Ni wazi kwamba suala la rushwa katika Mahakama limeonekana ni sugu kutokana na kila mwaka mhimili huo kunyoshewa kidole ama na TAKUKURU au viongozi wakuu wa serikali. Kwa maana hiyo rushwa katika mahakama imekuwa sawa na hadithi ya 'alfu ulela ulela' ambayo haifiki tamati.

Kama alivyosema Rais juzi, ni vyema watendaji wa mahakama wakabadilika kwa kufuata maadili na kuviishi viapo vyao kwamba katika kutekeleza kazi zao watafanya kwa kuzingatia haki na watajiepusha na huba na upendeleo. Kwa mantiki hiyo, ni vyema wakatenda haki badala ya kukengeuka kwa sababu ya kuahidiwa donge nono na mwenye dau kubwa katika shauri husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Jamani Yanga imetuletea fainali, kazi kwetu mimi, wewe kunufaika

**UNAPOZUNGUMZIA** mechi ya kimataifa maana yake ni kwamba kuna fursa hasa kiuchumi. Hebu fikiri idadi ya mashabiki takribani 60,000 wanaoketi kwa wakati mmoja kwenye uwanja Benjamin Mkapa, wenye hadhi hiyo.

Achilia mbali wageni wanaowasili na vikosi vyao, wanafikia hotelini, watapata malazi, mlo, usafiri pia utahitajika na hata kutembelea maeneo mbalimbali baada ya mechi, ikiwamo maduka makubwa na hifadhi.

Watanzania ni wakati wa kufungua jicho la fursa kwa kuzifanyia kazi hususan wawekezaji wakubwa, wadogo na wa kati, ambao hata wanaweza kuwa wauzaji bidhaa ndogo za vimiminika.

Mei 28 mwaka huu, timu ya Yanga inatarajia kucheza mchezo wa nyumbani fainali za Kombe la Shirikisho Afrika na USM Alger ya Algeria.

Mchezo huo ambao utachezwa uwanja wa Benjamin Mkapa, ni wakati wa wazawa kuzifuata na kuzitumia fursa hizo kwa kuuza bidhaa za asili zenye upekee na kuwavutia wageni.

Wakati mechi hizo zinapochezwa mazingira ambayo ni tulivu ni muhimu kwa kuwa yatamvutia hata mgeni aliyekuja kuangalia mechi hiyo, kutamani kusalia nchini kwa mapumziko zaidi.

Hivi karibuni, Shirikisho la Mpira Afrika (CAF), lilitangaza kupokea rasmi ombi la pamoja kwa mataifa ya Afrika Mashariki kuandaa Kombe la Mataifa ya Afrika ya mwaka 2027.

Algeria, Botswana na Misri ni miongoni mwa mataifa ambayo yamewasilisha nia ya kuandaa michuano hiyo.

CAF itatangaza mshindi wa kuandaa mashindano ya 2027, Septemba, mwaka huu, pamoja pia na waandalizi wa mashindano ya mwaka 2025 baada ya Guinea kupokonywa haki za kuandaa Oktoba mwaka jana, kutokana na maandalizi duni.

Wakati nuo huo, ni wakati Wa nchi kuandaa mzingira bora ya michezo, ikiwamo kutojirudia kwa matatizo ya umeme kukatika au kuwa hafifu uwanjani, ili mgeni ajapo afurahie mazingira.

**Hivi karibuni, Shirikisho la Mpira Afrika (CAF), lilitangaza kupokea rasmi ombi la pamoja kwa mataifa ya Afrika Mashariki kuandaa Kombe la Mataifa ya Afrika ya mwaka 2027.**

Misri iliandaa mashindano ya mwaka 2019 wakati Algeria ikiandaa mashindano ya mwaka huu kwa wachezaji wanaoshiriki ligi za ndani maarufu CHAN, pamoja na kuandaa mashindano ya wachezaji wasiozidi miaka 17.

Hii ikiwa na maana kuwa mataifa haya mawili hayana changamoto ya miundo misingi bora ya kuandaa michuano.

Hadi kufikia mwanzoni mwa Mei, mwaka huu, Botswana ilifaa kuwasilisha ombi la pamoja ila Namibia ikajiondoa dakika za mwisho kutokana na changamoto za kifedha.

Hata hivyo, haijulikani ni kiasi gani cha uwekezaji kitahitajika kuruhusu kati ya Botswana au nia ya pamoja ya Afrika Mashariki kufanikiwa kuandaa mashindano ya mwaka 2027.

Hadi mwaka 2021, Kenya ilikuwa na uwanja mmoja tu ulioidhinishwa na CAF kuandaa mechi za kimataifa uwanja wa Nyayo.

Licha ya kuwa uwanja wa Moi Kasarani unamiliki jina la kimataifa, CAF ilisema haukuwa umeafikia viwango vya kuandaa mechi za kimataifa.

Kenya ilipokonywa haki za kuandaa mashindano ya CHAN 2018 miezi minne tu kabla ya fainali hizo kwa sababu viwanja kadhaa havikuwa tayari. Kenya pia iliwahi kupokonywa haki za kuandaa kombe la mataifa ya Afrika ya mwaka 1996 kutokana na sababu hizo.

Wakati nchi za Afrika Mashariki zikiwa na ndoto ya mechi hizo, nchi kama nchi pia iwe na mikakati yake ya kuitumia fursa iliyopo kwa kuanza na mechi za ndani za kimataifa ambazo ni chanzo cha mapato.

## Serikali kuanzisha kampeni chanjo wanyama wafugwao

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega (pichani), amesema serikali inatarajia kuanzisha kampeni ya lazima ya chanjo kwa wanyama wafugwao nyumbani.

Amesema hatua hiyo itasaidia kupunguza au kuondoa hatari ya asilimia 70 ya magonjwa ya milipuko kwa binadamu yanayotoka kwa wanyama.

Waziri Ulega alisema hayo jana alipotembelea Hospitali ya Taifa ya Rufani ya Wanyama iliyoko Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wakati wa maadhimisho ya 18 ya kumbukizi ya Hayati Edward Moringe Sokoine yanayofanyika chuoni hapo kuanzia jana hadi Ijumaa.

Alisema kwa sasa nchi inapaswa kuingia kwenye kampeni ya kuchanja mifugo ya kufugwa itakayosaidia kupunguza magonjwa ya milipuko kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Ulega alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia sera ya kuchanja kwa wanyama wafugwao kama ilivyo kwa binadamu kwa sababu karibu asilimia 70 ya magonjwa ya binadamu yanatoka kwa wanyama hasa wanyamapori ikiwamo Corona, Murburg, kimeta, homa ya mgunda.

Alisema kampeni ya kuchanja pia itasaidia kutoa ajira za muda mrefu na mfupi kwa wataalamu wa wanyama walioko nchini sambamba na vijana wanaosoma kwenye vyuo mbalimbali kutumia nafasi hiyo kujifunza kwa vitendo na nchi kupata wataalamu wengi zaidi wa masuala ya wanyama.

Aidha, Ulega alisisitiza vijana na wawekezaji nchini kuhakikisha wanajikita katika kilimo cha majani ya malisho ya mifugo kwa ajili ya biashara hasa majani aina ya Apha -alpha kutokana na majani hayo kuwa na masoko zaidi ya ndani na nje ya nchi ikiwemo nchi ya Saudi Arabia.



Akizindua maadhimisho hayo, Ulega alisema serikali imelenga kuwahamasisha vijana kujihusisha na shughuli za ufugaji kibiashara kwa kuanzisha vituo atamizi vinane kwa ajili ya vijana, huku ikipanga kuongeza vingine vinane kwa mwaka ujao wa fedha 2023/24 sambamba na kuiwezesha kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) kuzalisha chakula bora cha mifugo, kuzalisha ndama bora na kuboresha majike wazazi.

Alisema ikiwa vijana watajiunga na shughuli za ufugaji kibiashara itawasaidia sababu malighafi katika viwanda vya nyama nchini, itakuwa imeongezeka na kutoa fursa ya kujiajiri na kisha kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

Aidha, alitoa wito kwa sekta binafsi na washirika wa maendeleo kuendelea kujitokeza na kuunga mkono katika kuwawezesha vijana kushiriki kwenye shughuli za kilimo kwa kutoa msaada wa hali na mali ikiwemo mitaji ya fedha, vitendea kazi, mafunzo na teknolojia zitakazowawezesha kushiriki katika kilimo kwa tija na ufanisi.



Mkurugenzi Mkuu wa Foshan Free Electronic Appliances Co. Ltd, Hellen Sun (kushoto) na Meneja Mauzo wa Urhome Company Ltd ya Tanzania, Evance Munuo, wakitiliana saini mkataba wa ushirikiano wa kibiashara, wakati wa mkutano wa kibiashara kati ya Tanzania na China ili kujadili fursa za uwekezaji, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mpina aibana serikali wizi wa bil. 83/- za dawa, vifaa tiba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, amehoji mikakati ya serikali ya kutokomeza mtandao wa wizi wa dawa na vifaa vya afya nchini na hatua zilizochukuliwa kwa watumishi waliobainishwa kufanya ubadhirifu wa Sh. bilioni 83 za dawa na bidhaa za afya.

Akiuliza swali bungeni jana, Mpina alitaka kujua serikali inachukua hatua gani kwa wanaobainika kujihusisha na wizi huo na ni fedha kiasi gani zinapotea kwa mwaka kutokana na wizi huo.

"Tathmini iliyofanywa na Wizara ya Afya Novemba, 2021 ilibaini Sh. bilioni 83 za dawa na bidhaa za afya zilikuwa zimeibiwa. Je, serikali ilichukua hatua gani kwa watumishi ambao wamefanya ubadhirifu huo,"alihoji.

Alisema uwezo wa kusambaza dawa na vifaa tiba wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ni asilimia 59 na inatokana na malimbikizo ya madeni ya zaidi ya Sh. bilioni 259 na mtaji wa Sh. bilioni 563 na kuhoji serikali inatoa kauli gani ya kuwezesha MSD ili kuwa na uwezo mkubwa.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema suala la kupambana na wizi na ubadhirifu wa bidhaa za afya si la serikali pekee bali ni la watu wote.

Dk. Mollel alitaja mikakati inayotekelezwa na serikali katika kutatua tatizo la



wizi wa dawa na vifaa tiba kuwa ni pamoja na kufanya agenda ya ulinzi wa bidhaa za afya kuwa agenda ya kudumu katika vikao vya kamati za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya.

"Pia kujenga uwazi wakati wa kupeleka bidhaa za afya na kuwapa wakuu wa wilaya na wabunge nyaraka za makabidhiano ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya rejea, kuimarisha mifumo ya usimamizi wa bidhaa za afya ikiwamo kufunga mifumo ya kielektroniki pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara,"alisema.

Dk. Mollela alisema mpango mwingine ni kuimarisha kamati za usimamizi za vituo kwa kuzijengea uwezo kuhusu majukumu yao katika usimamizi wa bidhaa za afya.

"Wizara ilifanya uchunguzi wa ubadhirifu wa bidhaa za afya na taarifa kuwasilishwa kwenye semina ya wabunge na kupelekwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili kupata thamani halisi ya bidhaa zilizopotea," alisema.

Kadhalika, alisema TAKUKURU inaendelea na uchunguzi kuhusu watumishi waliofanya ubadhirifu huo na miezi miwili iliyopita walikuwa hatua za mwisho kuchambua kilichofanyika ili wahusika wachukuliwe hatua.

"Fedha zinazopitishwa Sh. bilioni 200 ni fedha za vifaatiba na dawa kwenye vituo vyetu na vikipata fedha vinapeleka MSD, sasa hilo la wapewe mtaji liliibuka kwenye bajeti yetu na Wizara ya Fedha imelichukua na wiki iliyopita tulikutana ili kuona namna MSD wapatiwe mtaji," alisema.


**HOTEL CONTINENTAL LIMITED**
**(REG. 6032)**

**EXTRACT RESOLUTION TO REVOKE A RESOLUTION TO THE WIND UP THE COMPANY VOLUNTARILY**

At the meeting of the Company dated 12th April, 2023, the members of the above-named company passed the following special resolution

1.That the winding up resolution to wind up the company voluntarily dated 17th November 2021 be and is hereby revoked and that the voluntary winding up of the company be and hereby cancelled with immediate effect.

2.That the Members accepts the resignation of Ayoub Mtafya of NexLaw Advocates as Liquidator of the Company for purposes of such winding up.

Dated this 22nd day of May 2023

Certified true extract

Pascal Matunda, Jr. (Chairman)

Betty Machangu (Secretary)

# Watumishi 10 halmashauri wafukuzwa kwa utoro

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATUMISHI 10 wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamefukuzwa kazi baada ya kukutwa na makosa mbalimbali ya kiutumishi.

Akitangaza uamuzi huo jana, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Morris Makoi, alisema Baraza la Madiwani limebariki kufutwa kazi kwa watumishi hao baada ya kupitia makosa ya kila mmoja na kujiridhisha kwamba hatua zilizochukuliwa na mwajiri wao ni sahihi na hakuna aliyeonewa.

"Hawa tumeridhia kuwafukuza kazi kwa kauli moja kwa sababu ya makosa mbalimbali yakiwamo ya utoro. Hatua zilizochukuliwa na mwajiri, yaani Mkurugenzi Mtendaji ni sahihi," alisema.

Kwa mujibu wa Makoi, waliofukuzwa kazi ni Ofisa Mtendaji wa Kata, Gwau Kirua na maofisa watendaji wa vijiji vitano ambao ni Frans Laswai, Peter Komba, Amas Mkumbo, Leonard Lyamboko na Elisonguo Shayo.

Wengine waliofukuzwa kazi na nafasi zao kwenye mabano ni Dastan Mhando (dereva), Riziki Abdalla (ofisa kilimo), Joyce Kidalo (ofisa muuguzi msaidizi) na Sophia Mwakyima (muuguzi).

Aidha, Mwenyekiti huyo alisema watumishi watatu waliokuwa wamesimamishwa kazi, wamerejeshwa baada ya kuonekana hawana hatia. Watumishi hao ni Flavian Matemu (ofisa elimu kata), Ramla Hamis (mtunza kumbukumbu) na Christina Mbando (msaidizi wa ofisi).

Kutokana na kadhia hiyo, Makoi ameonya kuhusu nidhamu kazini na makosa ya utoro, akisisitiza ni nyema kila idara watumishi wake wakajitathmini juu ya utendaji kazi wao.

"Wako baadhi ya watendaji wa vijiji, ambao hawasomi mapato na matumizi kwa wananchi. Naagiza kuanzia sasa itisheni mikutano ya hadhara na kuwasomea wananchi mapato na matumizi, kwa kuzingatia kanuni.

"Tunataka wananchi watambue fedha zinazokusanywa katika kijiji chao zinafanya nini. Lakini tunataka walimu wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri yetu, wahakikishe wanafika katika vituo vyao vya kazi kwa wakati na kuachana na tabia za utoro na uzembe wawapo kazini," alisema.




Naibu Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Melissa McNeil Barrett, akizungumza katika makabidhiano ya kituo cha huduma shufaa na ofisi ya Polisi Dawati la Jinsia Wanawake na Watoto, Bugarama, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga jana. Shirika hilo, limejenga vituo hivyo kwa ushirikiano wa UN WOMEN kwa ufadhili wa shirika la ushirikiano wa kimataifa la serikali ya Korea Kusini (KOICA). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Jela miaka 150 kwa kuwanajisi wanawe

**Na Jaliwason Jasson,** KITETO

BABA mzazi wa watoto watano wa kike, Jackson Ole Naiko (57), Mkazi wa Ndareta, Kiteto mkoani Manyara, amehukumiwa kifungo cha miaka 150 jela baada ya kupatikana na hatia ya kuwanajisi watoto wake.

Ole Naiko alihukumiwa kutumikia adhabu hiyo juzi na Mahakama ya Wilaya hiyo, baada ya kumtia hatiani.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Kiteto, Mossi Sasy, alisema mshtakiwa ametiwa hatiani kwa kosa la kuwanajisi watoto wake wa kuwazaa kwa nyakati tofauti.

Mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 158 (1) (a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya sheria iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

"Baada ya mahakama hii kumtia hatiani mshtakiwa, ina mhukumu kutumikia adhabu ya miaka 30 kwa kila kosa na kuwalipa fidia ya shilingi milioni moja kwa kila mtoto," alisema Hakimu Sasy.

Mshtakiwa huyo alikuwa akikabiliwa na kesi namba mbili, tisa, 10, 11 na 12 za mwaka 2022.

Kwa mujibu wa Hakimu Sasy, katika kila kesi, upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi saba wakiwamo watoto, mama zao, daktari na askari polisi ambao walitoa ushahidi ambao haukuacha shaka ndani yake.

Katika hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani hapo, Mwendesha Mashtaka, Joseph James, alidai kuwa mshtakiwa alikuwa akizini na watoto wake kwa nyakati tofauti wakiwa nyumbani au shambani, huku akiwatishia kuwadhuru kama watatoa siri hiyo.

Kutokana na makosa hayo, mwendesha mashtaka huyo aliiomba mahakama hiyo, kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine katika jamii.

**Baada ya mahakama hii kumtia hatiani mshtakiwa, ina mhukumu kutumikia adhabu ya miaka 30 kwa kila kosa na kuwalipa fidia ya shilingi milioni moja kwa kila mtoto.**

# Serikali kutafiti uwezo kulipa pensheni wazee

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema serikali itafanya utafiti wa kina kwa lengo la kubaini uwezo wa kulipa pensheni kwa wazee wote.

Hata hivyo, kwa sasa serikali imekuwa ikihudumia wazee kutoka katika familia au kaya zenye umaskini uliokithiri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Katambi alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Hawa Mchafu.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali imeishia wapi kuhusu mchakato wa pensheni kwa wazee wote.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema pensheni kwa wazee wote inajumuisha wale ambao walikuwa katika ajira ambao kwa sasa wanalipwa pensheni na mifuko waliyochangia wakati wanafanya kazi na pili wazee ambao hawajawahi kuajiriwa kwa sasa hawalipwi.

"Mchakato wa kuwalipa pensheni wazee wote ambapo utajumuisha wazee ambao hawajawahi kuajiriwa ni utaratibu mpya ambao utahitaji kugharamiwa na bajeti ya serikali,"alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asha Abdullah Juma, alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wazee waliostaafu kwenye Shirika la Posta Tanzania, Shirika la Reli Tanzania na Shirika la Ndege Tanzania, wanalipwa pensheni zao.

Akijibu swali hilo, alisema madai mbalimbali ya wazee waliofanya kazi kwenye mashirika hayo kuna ambao wamelipwa na wengine bado wanadai kutokana na kutokuwapo kwa taarifa sahihi za madai hayo na kusisitiza serikali bado inaendelea kufanya ufuatiliaji ili wapate stahiki zao.



# Shule ya St. Mary Goreti kuotesha miti 2,000

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari St. Mary Goreti iliyoko Moshi mkoani Kilimanjaro, imepanga kuotesha miti 2,000 mkoani humo ili kuunga mkono juhudi za serikali za kupanda miti na kurudisha uoto wa asili.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa shule hiyo, Sr. Clementina Kachweka wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kupanda miti iliyofanyika katika viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

"Mpango huu wa kupanda miti utakuwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa shule yetu yanayotarajiwa kufanya mwakani, kwamba tunashirikiana na Benki ya NMB ambayo imechangia miche 1,000 kati ya 2,000," alisema.

Alisema ili kutimiza adhma hiyo, shule hiyo inatarajia kugawa miti katika wilaya zote za Mkoa wa Kilimanjaro ambayo itapandwa maeneo mbalimbali kwa utaratibu utakaowekwa na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

"Kama tunavyojua, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango alitangaza kuwa upandaji miti uwe ni kipaumbele cha kwanza hapa nchini, hivyo katika kuunga mkono juhudi za serikali, tumeingiza mpango wa kupanda miti kama sehemu ya maadhimisho yetu ya miaka 25 ya shule yetu," alisema.

Alitoa rai kwa wananchi wote kuunga mkono juhudi za serikali za kupanda miti kutokana na ukweli kuwa miti ni sehemu ya maisha ya binadamu.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori, aliupongeza uongozi wa shule hiyo kwa kuja na mpango wa kupanda miti na hivyo kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha mazingira na kurudisha uoto wa asili.

"Upandaji wa miti 4,000 ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro ni hatua kubwa katika kuboresha mazingira na pia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa ni changamoto kubwa katika miaka ya hivi karibuni," alisema.

Alisema kuwa maboresho ya mazingira ni muhimu kutokana na ukweli kwamba ndiyo chanzo cha ubora wa maisha ya wanadamu kwa njia moja au nyingine.

Hivyo alitoa rai kwa taasisi zingine za kielimu, taasisi binafsi ikiwamo za umma na wadau wengine wa maendeleo kuiga mfano wa Shule ya St Maria Goreti kwa kuanzisha kampeni za upanda miti na utunzaji wa mazingira kwa ujumla ili kuboresha mazingira kwa kurudishia uoto wa asili.

Wakati wa hafla hiyo, Makori na Mkuu wa shule hiyo, Sr Clementina, walipanda mti mmoja kila mmoja ikiwa ni ishara ya uzinduzi huo ambao pia ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali ngazi ya mkoa na wilaya, viongozi wa shule hiyo, walimu, wafanyakazi na wanafunzi.

**Maboresho ya mazingira ni muhimu kutokana na ukweli kwamba ndiyo chanzo cha ubora wa maisha ya wanadamu kwa njia moja au nyingine.**

# Serikali yatoa milioni 306/- ujenzi shule ya msingi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI kupitia mradi wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za awali na msingi (BOOST), imetoa Sh. milioni 306.9 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi katika Kijiji cha Lemanda Kata ya Oldonyosambu, Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru.

**Kujengwa kwa shule hiyo kutapunguza adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu wa kilomita 20.**

Akizungumza jana kwa niaba ya wananchi wa kijiji hicho wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Emanuely Laizer, alisema kukamilika kwa shule hiyo itakuwa mkombozi kwa watoto wa eneo hilo.

Alisema wanafunzi wa kijiji hicho walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata elimu kwenye vijiji na kata za jirani, hivyo ujenzi huo utakuwa mkombozi kwa wanafunzi kwa kuwa watapata elimu karibu na makazi yao.

"Kwa kweli tunaishukuru serikali kwa kutoa fedha za ujenzi wa shule hii kwa kuwa watoto wetu walikuwa wanatembea umbali mrefu kwenda kufuata elimu kwenye vijiji na kata za jirani yetu na tunaamini mradi huu utakuwa mkombozi kwa kijiji chetu," alisema.

Mkazi mwingine Seuri Lesuroi, alisema hakuwahi wala hakupata fursa ya kusoma jambo ambalo linamuumiza hadi leo, kwamba hata watoto wake waliteseka kwa kutembea kwenda shuleni.

"Kinamama wa Lemanda tumefurahi kujengewa shule hapa kijijini kwa kuwa watoto wetu waliteseka kwa kutembea umbali mrefu hata sisi wazazi hatukuwa na amani pale wanapokwenda shuleni hasa kipindi cha mvua, hivyo kwa ukaribu huu wa shule tutakuwa na amani," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Oldonyosambu, Raymond Lairumbe, alitoa pongezi kwa serikali kwa kupeleka mradi kwenye kijiji hicho akisema unakwenda kutimiza ndoto za watoto wa jamii ya kifugaji kwenda shule.

Hata hivyo alisema kujengwa kwa shule hiyo kutapunguza adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu wa kilomita 20.

"Shule hii tumeipa jina la Naisula ikimaanisha ushindi uliopitiliza hakika kuwapo kwa shule hii ni ushindi kwa watoto wa Lemanda na jamii nzima ya wafugaji kwa awali walishindwa kupata fursa ya elimu kutokana na kutembea umbali mrefu.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Oldonyosambu, Joseph Saria, aliishukuru serikali kwa kutekeleza kwa vitendo ilani ya chama hicho kwa kuwa watoto wao watasoma kama wengine.

Pia alisema kutokana na ujenzi huo wasichana wataacha kuolewa kwa kuwa watapenda masomo, huku wavulana watasitisha mpango wa kutoroka kwenda nchi ya jirani kwa ajili ya kufanya kazi za ulinzi.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Willy Mwamasika, akitoa elimu kwa madereva na makondakta kuhusu wajibu wao kazini katika stendi kubwa ya mabasi yaendayo mikoani, Kange jijini Tanga juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# 'Madereva wana mchango kukuza uchumi'

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Willy Mwamasika, amesema madereva wamekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha na kukuza uchumi, kwamba wanawajibu wa kufanya kazi kwa weledi ili kuepusha madhara kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na madereva pamoja na utingo katika Stendi Kuu ya Mabasi Kange kwa dhamira ya kuwakumbusha wajibu wao wakiwa kazini.

"Kila mtu ana nafasi yake katika uchangiaji wa uchumi kwa hiyo kupitia kazi mnayofanya mna mchango katika ukuaji wa uchumi wa Tanga, il imradi utendaji kazi wenu mhakikishe hamvunji sheria kwa kuwa mnabeba abiria na kuwapeleka katika majukumu yao.

"Mna wajibu wa kuchukua tahadhari zote mnapokuwa barabarani kwa kuhakikisha hamleti madhara kwa abiria kwa kuwa madereva mnapaswa kuendesha vyombo vya usafiri kwa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa hasa sheria ya usafirishaji. alisema," alisema.

Aidha, aliwataka madereva hao kufanya kazi kwa weledi kuepuka usumbufu wa askari wa barabarani kwa kuwa itamsaidia kila mmoja kuwa na uhuru anapokuwa katika eneo lake la kazi.

Vilevile alipiga marufuku kwa mawakala wanaotafuta abiria na kuwafanyia usumbufu kwa kuwavuta na kuwasababishia kero kwa kuwa wako baadhi ambao ni vibaka wanakwenda stendi kwa ajili ya kuwaibia watu.

Pia alitoa rai kwa madereva wanaoendesha vyombo vya moto kwa mwendo wa kasi wafuate maelekezo ya serikali kwa kutembea mwendo wa kawaida.

"Tembeeni mwendo unaotakiwa kwa kuwa kwa sasa dunia ni kama kijiji usije ukasema hatukuoni huko barabarani, uliko na sisi tuko, kwa atakayekiuka agizo atapigwa faini, atafikishwa mahakamani au kufungiwa leseni na endapo atafunguliwa leseni atalazimika kuanza upya utaratibu wa kuomba," alisema.

Kadhalika alisema kwa madereva wa mabasi makubwa na daladala wenye leseni za madaraja ya C na E, kuwa kazi ya uhakiki wa leseni hizo unaendelea lakini baada ya muda kupita serikali itaanza msako wa kuwakamata ambao hawajahakikiwa.



# Waomba kikosi maalumu kudhibiti uvuvi haramu

**Na Rose Jacob,** UKEREWE

BAADHI ya wananchi wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, wameiomba serikali kupeleka kikosi maalumu kwa ajili ya kukabiliana na uvuvi haramu.

Wamesema wanaohusika ni baadhi ya watu wakiwamo viongozi wa ngazi mbalimbali hali inayosababisha upungufu wa samaki.

Walieleza hayo kwa nyakati tofauti baada ya kupigwa marufuku kwa baadhi ya mitego inayotumika kinyume cha sheria katika Ziwa Victoria yakiwamo makokolo.

Makokolo hayo yamekuwa yakikamatwa na kufikishwa pungufu katika maeneo husika kutokana na wamiliki wake kuwa miongoni mwa viongozi wa ngazi mbalimbali serikalini.

**Wanaohusika ni baadhi ya watu wakiwamo viongozi wa ngazi mbalimbali hali inayosababisha upungufu wa samaki.**

Mkazi wa Nansio, Suzaba Mafuru: "Tunaiomba serikali kuwachukulia hatua kali watumishi wa umma wanaojihusisha na vitendo vya uvuvi haramu maana wao wamekuwa chanzo cha hali hiyo kuwa endelevu, vifaa vikikamatwa kwa ajili ya kuteketezwa wanatunza na kupeleka vichache na uvuvi huo unaendelea ni bora kiwepo kikosi maalumu ambacho kitakuwa msaada juu ya tatizo hili."

Aidha waliiomba serikali kuwa na utaratibu wa kuwahamisha kila baada ya muda watumishi wa sekta ya uvuvi kutokana na viongozi wa idara hizo kuyazoea mazingira baada ya kutumika maeneo husika kwa kipindi kirefu.

Nao baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo wakizungumza wakati wa kikao cha kawaida walisema hali ya udhibiti uvuvi haramu bado iko chini hivyo kuishauri serikali itenge watu maalumu watakaopambana na suala hilo.

"Maofisa uvuvi wamezidiwa na jukumu hilo hivyo kusababisha uvuvi haramu, unaoua samaki wachanga na mazalia ya samaki ambayo yakitoweka yataleta shida ya uchumi kwa wananchi na serikali kwa ujumla maana hiki ndicho chanzo chetu kikuu cha uchumi," alieleza Diwani John Ndaro.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Joshua Manumbu, alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali wawe nguzo kuu ya kupambana na uvuvi haramu na kueleza kuwa kuna baadhi ya viongozi wanamiliki makokolo.

Alisema baadhi ya viongozi hao wamewapa ndugu zao makokolo, wanayatumia katika uvuvi.



Meneja Mawasiliano wa Hospitali ya CCBRT, Abdul Kajumulo (wa pili kushoto), akikabidhi vipeperushi vyenye ujumbe kuhusu fistula ya uzazi kwa Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Isaac Mwakisu, wakati wadau wa mapambano dhidi ya fistula ya uzazi walipomtembelea ofisini kwake, katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya kutokomeza fistula ya uzazi duniani, wilayani humo, mkoani Kigoma juzi. Wanaoshuhudia ni Yohana Kasawala kutoka CCBRT (kushoto), Dk. Jonas Kagwisage kutoka Americare (kulia) na Clement Ndahani kutoka Fistula Foundation (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAWA yatakiwa kutoa elimu kujikinga na wanyama hatari

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imetakiwa kutoa elimu kwa wananchi ambao wanaishi kando ya Ziwa Victoria juu ya kujikinga na wanyama hatari waishio majini.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Sengerema, Mark Makoye, baada ya ongezeko la matukio ya mara kwa mara ya wananchi kushambuliwa na wanyama hao wakati wakifanya shughuli zao za kila siku.

Alisema wananchi wa Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema hawana elimu ya kujikinga dhidi ya wanyama wanaoishi majini licha ya shughuli zao nyingi kutegemea Ziwa Victoria.

Akieleza juu ya suala hilo Ofisa Uhifadhi Daraja la Kwanza, Mhamed Omar kutoka TAWA Kanda ya Ziwa, alisema wananchi wamekuwa wakihusisha mashambulizi ya mamba na masuala ya kimila hali inayosababisha kushindwa kufuata ushauri wa mamlaka husika.

Aidha alieleza kuwa suala la elimu bado linafanyiwa kazi na wamekuwa wakiwaeleza wakazi wa maeneo hayo kuhakikisha wanafanya shughuli zao kwa tahadhari, wakiwa katika makundi kwani wanyama hao hawawezi kukaa maeneo yenye kelele za watu.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Buchosa, Idama Kibanzi, aliwaagiza madiwani kwa nafasi zao kutoa elimu kwa wananchi kuachana na mitazamo ya kizamani ambayo huwaaminisha kuwa wanapooga maji ya ziwani wanatakata kuliko kuchota na kwenda kuogea nyumbani.

Alisema hali hiyo inayosababisha baadhi yao kuvamiwa na wanyama hao wakali.

Katika kipindi cha Julai 2022 mpaka Mei 2023 watu 11 wamefariki dunia kwa kushambuliwa na mamba na wengine wanne kujeruhiwa, watu 117 mazao yao ya chakula yakiharibiwa na wanyama.

# NEMC kuzigeukia nyumba za ibada zinazopiga kelele

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BARAZA la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) limewataka viongozi wa makanisa kuendelea kufuata sheria, kwamba watakaokiuka watafungiwa.

Hatua hiyo imekuja baada ya kufanyika kwa operesheni ya kufunga shughuli za muziki katika kumbi za starehe pamoja na baa zinazozalisha kiwango kikubwa cha kelele mkoani hapa.

Hayo yamebainishwa jana na Meneja wa NEMC Kanda ya Ziwa, Kayombo Jarome, wakati akitoa ufafanuzi juu ya kufungiwa kwa shughuli za muziki katika baa na sehemu za starehe zilizokiuka utaratibu mkoani humo.

Kayombo alisema operesheni hiyo ni takwa la kisheria kufuatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 106 Ibara ya 5 na 6 ya mwaka 2014 na wote ambao wamefuata taratibu ikiwa ni pamoja na kulipa faini kwa mujibu wa sheria, kuweka vifaa vya kupima sauti pamoja na kusimika mifumo ya kuzuia kusambaa kwa sauti tayari wamefunguliwa na kuruhusiwa kuendelea na shughuli zao.

Aidha, alisema kuwa semina mbalimbali za kuelimisha wamiliki wa sehemu hizo zimekuwa zikifanyika mara kadhaa na hatua hiyo siyo ya kushtukiza bali waliofungiwa wote walikuwa wanajua utaratibu na wakaamua kukiuka kwa makusudi.

Alieleza kuwa baada ya hatua hiyo NEMC watakaa na viongozi mbalimbali wa dini lengo likiwa ni kuwataka kufuata sheria na taratibu za kelele katika mazingira na wote watakaoendelea kukiuka utaratibu huo watachukuliwa hatua za kisheria bila kujali shughuli husika.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Masala, alisema katika mkoa huo kaguzi 50 zimefanyika na baa 31 zilikutwa na makosa ya uzalishaji kelele kwa kiwango cha juu na hakuna hoteli iliyokutwa na makosa wala kufungiwa.

Masala alisema: "Ieleweke kuwa ni mziki pekee uliofungiwa na siyo eneo husika hivyo shughuli nyingine zinaendelea katika baa hizo, pia waliolipia faini na kufuata utaratibu wanaendelea na shughuli zao na faini inayotozwa ipo kisheria na inatozwa kuanzia Sh. milioni 200 kwa baa iliyofanya makosa hayo kwa kujirudia inatozwa Sh. milioni tano."


**Katika mkoa huo kaguzi 50 zimefanyika na baa 31 zilikutwa na makosa ya uzalishaji kelele kwa kiwango cha juu na hakuna hoteli iliyokutwa na makosa wala kufungiwa.**

ama
ALHAMISI MEI 25, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



## Kasi shinikizo damu, miaka mitano ongezeko ni mara mbili ya zamani

Ukurasa 12



## Atafiti akugundua viumbe kutoweka nchini, atunukiwa udaktari heshima

Ukurasa 14

# MKUTANO RASILIMALI WATU AFRIKA...

# Mwenyeji Samia adokeza Tanzania iko pazuri, mzizi kwenye afya umma

**Mwandishi Wetu**

NI siku chache zimepita, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amezindua maandalizi ya mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika, kuhusu uwekezaji rasilimali watu na kujibu hitaji la nguvu kazi hiyo utakaoanza leo, ukidumu kwa siku mbili.

Taarifa ya Benki ya Dunia iliyosambazwa juzi, ikamnukuu Rais Dk. Samia kuhusu nafasi ya viongozi wa Afrika, waunda sera na wadau wa maendeleo kwa ujumla, kufuatilia afya na stadi za watu walioko kazini.

Hilo linafanyika, huku Makamu Rais wa Benki ya Dunia, Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa akitaja matarajio ifikapo mwaka 2050, idadi ya watu itaongezeka mara mbili kufika bilioni 2.2, ilhali imeingia katika karne iliyoko na pengo la nguvukazi inayojimudu.

Kimsingi, Rais Dk. Samia anapozungumzia maendeleo ya nguvukazi, kwa sura ya awali ina maana ya mtaji kiuchumi, lakini nyuma ya pazia kunakobeba picha pana na kuu inaangukia uchumi.

Mzizi wa taasisi rasilimali watu (human resource), inasimamia sura ya ubunifu au kujiongeza, ikiwa ndiye mkuu katika yote ya uzalishaji na uotaji huduma, ikihama kutoka kwenye mtendaji (personell).

Ni dhana iliyoibuliwa kitafiti kuanzia mizizi ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani (IMF) na wadau wa kimataifa, zikiamini rasilimali watu ndio wanaozalisha na kuendesha nyenzo zingine za uzalishaji, kama mtaji fedha na miundombinu.



Mwalimu ni sehemu muhimu kitaifa katika kuzalisha rasilimali watu bora. **PICHA: MAKTABA.**

Ili rasilimali watu kuwa na tija, inapaswa kuwapo uwekezaji ndani yake ikiisimamia zaidi afya, ndio vingine vinafuata kama vile elimu, huduma na sera. Hapo ndipo hoja na nafasi ya Rais Dk. Samia anatoa tangu anaingia madarakani.

Kwenye msingi wa afya, kuzalisha tija ya kutoka kwa binadamu inaanzia kwenye siku 100 za kiumbe kinapozaliwa, kupata malezi na huduma sahihi za kiafya.

Tanzania ikiwa katika nafasi ya utendaji wake kiuongozi, kumekuwapo staili ya kupokezana vijiti kwenye kivuli cha chama kinachotawala hadi sasa na kwa maana hiyo, wanasimama katika sera inayofanana, tofuati ni katika falsafa ya mkuu wa nchi aliyepo, maono, kadhalika mahitaji ya wakati.

Tangu kuingia kwake madarakani zaidi ya miaka miwili iliyopita, Rais Dk. Samia akiwa mkuu wa nchi na kabla ya hapo zaidi ya miaka mitano, makamu mkuu wa nchi ana mengi katika kufanikisha kuandaa nguvu kazi.

Ushuhuda unaanza katika namna akitumikia awamu ya tano makamu rais na rekodi ya sasa, kisha mkuu wa nchi, sasa ikiwa ni miaka mitano na ushee akipiga hatua kubwa kuneemesha rasilimali watu wa sasa na wajao.

**DK.SAMIA NA MMAM**

Mzizi wake unaanzia, Rais Dk. Samia katika uongozi wa awamu ya sita kwenye 'kijiti' cha Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ulioasisiwa katika awamu ya nne, chini ya Rais Jakaya Kikwete umekuwa na mtazamo mpana.

Tangu wakati huo kumetengwa kila kijiji au kitongoji kuwa na zahanati, kituo cha afya kwa kata na ngazi zote za juu ni kuwa na hospitali, kuanzia mkoa na zaidi kuwapo hospitali za rufani.

Hiyo yote imebeba maana ya kusogezea tija ya kiafya Mtanzania kuanzia anayezaliwa, aliye masomoni, kazini hadi mstaafu, mfano hai unaoendelea wa kampeni za kuwapo chakula kwa wanafunzi shuleni, ili kupatikana tija darasani. Hao ndio nguvu kazi kwa kipindi kijacho, ambao wana historia ya tija kwa siku zao 100 za uhai.

Hapo inapoongezewa na elimu bora, hali kadhalika sera na huduma sahihi, inatoa majibu kwa tija ya rasilimaliwatu kitaifa, ikishuhudiwa fursa zake zikipanuliwa kwa namna endelevu, mfano maboresho yanayofanyikia katika mrejesho wa mikopo elimu ya juu.

Kwa namna ya upekee, Rais Dk. Samia, ndani yake akaingiza juhudi ambazo zinapanua fursa ya kijinsia katika uongozi kitaifa, nafasi za wanawake zikipanuka kwa kasi.

Ni wiki hii Rais Dk. Samia, akaweka wazi namna anavyopanua idadi ya majaji katika ngazi ya mahakama kuu, ikiwa inakaribia uwiano kufikia asilimia 50.

Katika juhudi hizo za rais wa awamu ya sita, mtangulizi wake wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete akavunja ukimya, akitoa rai kwa Watanzania kumuombea Rais Dk. Samia, ili aendelee kuwa na afya njema na kuwatumikia wananchi kwa kutatua changamoto zina-

Inaendelea Uk. 12

## MWENYEJI SAMIA ADOKEZA TANZANIA IKO PAZURI, MZIZI KWENYE AFYA UMMA

Inatoka Uk. 11

zowakabili.

Kikwete akiwa mjini Kibaha mnamo katikati ya mwezi uliopita, iliyoandaliwa na Rais Dk, Samia kwa ajili ya wananchi wa mkoa wa Pwani, akitamka:"Kazi aliyo nayo Rais (Dk. Samia) ni kubwa. Inahitaji hekima na juhudi nyingi, hivyo ili kufikia malengo anapaswa kuongozwa na Mungu, sisi sote ni vyema tukamuombea,"

**ANAVYOTETEA AFYA**

Rais Dk. Samia akafafanua, chapicho la kitabu 'Tanzania Nutritional Survey' la mwaka 2019, udumavu kwa watoto wenye chini ya umri miaka mitano ulikuwa asilimia 31.8; wenye uzito pungufu asilimia 15; ukondefu asilimia 3.5.

Vivyo hivyo akarejea, hali ya lishe kwa wajawazito katika ngazi ya kujifungua inaonesha upungufu wa damu asilimia 28; huku utapiamlo uliokithiri unaendelea kuongezeka kufikia asilimia 31.8, wote wakiangukia zao la nguvu kazi kwa wakati tofauti.

Hapo ana nena katika zama za uongozi wake kuwa: "Nafurahi kueleza kwamba juhudi zinazofanywa na serikali kwenye suala la lishe, ikiwamo kutoa elimu kuhusu masuala ya lishe, kutenga mafungu maalum kwa halmashauri, kuongeza virutubishi kwenye chakula na kuwapa dhamana wakuu wa mikoa kusimamia masuala ya lishe kwenye maeneo yao, kumeboresha hali ya lishe ingawa jitihada zaidi zinahitajika."

Katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Rais Dk. Samia anafafanua vijana ni nguvu kazi muhimu kuweka nguvu za pamoja, serikali ikiendelea kutoa elimu, sambamba na kukabili ugonjwa Ukimwi na Virusi vya Ukimwi.

Akiwa ziarani mkoani Geita, Rais Dk. Samia, akatilia mkazo hoja ya maboresho ya rasilimali watu nchini, kwa kuwataka Watanzania kujiunga na bima ya afya kwa wote pindi itakapoanza ili wanufaike nayo, huku serikali ikiboresha huduma za afya nchini.

Ni hatua inayogusa pia kinamama na hali ya kijinsia, pale raslimaliwatu yao shuleni inapopata mimba, amewaandalia utaratibu unaowapa fursa kurejea masomoni.

Mkutano wa uwekezaji rasilimali watu unawaleta pamoja wakuu wa nchi na serikali za Afrika kubadilishana uzoefu na kutoka na azimio la pamoja juu ya namna ya kuboresha uwekezaji huo barani Afrika.

AFYA

# Kasi shinikizo damu, miaka mitano ongezeko ni mara mbili ya zamani




Waziri Ummy Mwalimu, akifanya vipimo katika maadhimisho ya Siku ya Shinikizo la Juu la Damu, Jijini Dodoma. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

MAGONJWA yasiyoambukiza, sasa yanasumbua rika zote, kukitajwa shida kama za kansa, kifafa, moyo, kisukari, pumu na presha.

Ni magonjwa yanayochangiwa na mfumo wa mlo na kuna wengine wanayarithi katika uhusiano kimaumbile. Kwenye mlo kunatajwa vyakula vyenye mafuta mengi, mwili kutofanya mazoezi na wengine inatokana na uzito uliokithiri.

Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa jamii jinsi ya kujilinda dhidi ya magonjwa hayo na mtu anapochelewa kupata matibabu, huweza kumletea ulemavu au kupoteza maisha kwa kutegemea ukubwa wake.

Hicho huifanya jamii iwajibike kujenga utaratibu wa kuchunguza afya zao na wanapobainika kuwa na magonjwa yasiyoambukiza, iwe rahisi kupata matibabu haraka.

Ni hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema shinikizo la juu la damu wagonjwa wake wameongezeka kutoka 688,901 nchini mwaka 2017 hadi 1,345,847 mwaka 2021, sawa na ongezeko asilimia 95.4 katika miaka mitano.

> **"Mpango wa serikali kupitia Wizara ya Afya, ni kutoa mafunzo ya utoaji huduma za magonjwa yasiyoambukiza...**

Waziri Ummy anatamka hayo jijini Dodoma, katika maadhimisho ya Siku ya Shinikizo la Juu la Damu Duniani, akifafanua: "Takwimu hizi zinatuonyesha kwamba wagonjwa hawa wenye shinikizo la damu wameonekana kuongezeka takribani mara mbili zaidi kwa kipindi cha miaka mitano."

Ummy anafafanua, magonjwa yasiyoambukizwa yameongezeka kwa asilimia 9.4 na kwa miaka iliyopita 2017 hadi 2021 kwenye vituo vya afya nchini. Wagonjwa hao wameongezeka hadi kufikia 3,440,708 kwa mwaka 2021.

Anafafanua, takwimu zinaonyesha watu watatu hadi wanne kati ya 10, wana shinikizo la juu la damu, kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa kwenye mikoa ya Pwani, Arusha, Geita, Mtwara, Lindi, Zanzibar, Iringa na Dar es Salaam.

Waziri Ummy anataja mikakati ya kutatua, wizara imeruhusu dawa za kukabili shinikizo la juu la damu katika ngazi ya msingi kuruhusiwa dawa mpya aina tatu, akizitaja ni; Losartan, Amlodipine na Hydralazine, zitumike katika kituo cha afya na dawa mbili; Nifedipine na Frusemide, kutumika zahanati.

"Mpango wa serikali kupitia Wizara ya Afya, ni kutoa mafunzo ya utoaji huduma za magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo huduma za ugonjwa wa shinikizo la damu, kwa watoa huduma 2400 kutoka vituo vya afya vyote 600 katika mikoa yote 26," anasema.

Anataja aina mbili za shinikizo la juu la damu, la asili, pia linalosababishwa na magonjwa mengine. Hapo anaeleza: "Inakadiriwa asilimia 90 hadi 95 za watu wanaathiriwa na shinikizo la juu la damu la asili, yaani wana ugonjwa huu bila kuwa na chanzo cha kisayansi kinachofahamika."

Anasema shinikizo la juu la damu linalosababishwa na magonjwa mengine hutokana na magonjwa ya figo, mapafu, mfumo wa homoni huathiri asilimia tano hadi 10 na iliyobaki ya watu wenye shinikizo la juu la damu.

Waziri Ummy anawakumbusha Watanzania, umuhimu wa kubadili mtindo wa maisha, kwa kuzingatia mazoezi, kuepuka tabia bwete, kuepuka matumizi ya tumbaku na bidhaa zake na kupunguza vilevi.

"Tuzingatie ulaji unaofaa wa mlo kamili wenye mboga mboga na matunda ya kutosha ili kuimarisha kinga ya mwili dhidi ya magonjwa, kupunguza matumizi ya chumvi, sukari na vyakula venye mafuta mengi, pamoja na kuzingatia unywaji wa maji ya kutosha angalau kiasi cha lita 1.5 ya maji kwa siku." anashauri.

MAZINGIRA

# TFS kurejesha hekta milioni 5.2 kuhusiana na uoto wa asili

**Na Jenifer Gilla**

DUNIA inapitia changamoto mbalimbali za kimazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi tangu mwaka 1979, kwa mujibu wa vyanzo vya kimataifa.

Kutokana na hali hiyo, ikabainika kuwapo ongezeko la joto duniani, hali inayolazimu kuchukuliwa hatua za kukabiliana na hali hiyo, kwa kufanya jihitada mbalimbali.

Aidha, katika hilo kunaonekana shughuli za binadamu zinachangia ongezeko la athari hiyo hivyo kwa kuwa wanaondoa uoto wa asili ili kutimiza mahitaji yao ikiwamo kukata misitu ambayo inatoa hewa ya oksijeni inayofanya kazi kubwa ya kusafisha hewa ya ukaa ambayo kuchangia kuwapo joto la kupitiliza.

Miaka 10 nchi wanachama wa kukabiliana na mabadililiko ya tabianchi ilifanya mkutano mjini Bonn Ujerumani uliopewa jina la Bonn Challenge ulioweka azimio ifikapo mwaka 2030 iwe imefanya jitihada za kurejesha uoto takribani hekta milioni 350 duniani ambazo aidha zinaweza kupotea au zimeharibika zirejeshewe uoto wake.

Katika mkutano huo Afrika ikiwa na nchi wanachama 54 iliahidi kurejesha hekta milioni 100 ndipo ikaja na mkkakati waliouita AFRI 100 yaani Afrika 100, ikiwa na maana ya hekta ambazo bara hilo limeweka azimio la kufikia.

Baada ya kufikia azimio hilo Afrika ikazitaka nchi wanachama na zenyewe ziweke maazimio na malengo yao ya kiasi gani kila nchi itachangia kufikia hekta hizo ambapo kati ya nchi hizo 32 zimesaini mkataba na kuingia katika utekelezaji wa uoto huo.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoingia kwenye mkataba wa urejeshaji wa uoto wa asili na kujiwekea malengo ya kurejesha uoto huo wa asili kwa hekta milioni 5.2 mpaka kufikia mwaka 2030 ili kufidia hekta 469,000 zilizopotea.

Wakala wa Misitu Tanzania wakiwa ndio wawakilishi wa nchi katika mkakati huo wamebeba jukumu zima la kuhakikisha kuwa liwike ama lisiwike, idadi hiyo ya uoto wa asili lazima iwe imepandwa hadi kufikia mwaka huo kama walivyoahidi.

Akizungumza na wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) wiki iliyopita, Mkuu wa Sehemu ya Utangazaji Utalii Ikolojia wa TFS, Anna Lauwo, alisema tayari mipango imeshaanza ikiwamo kuandaa mkakati wa namna watakavyorejesha uoto huo, kwa kushirikiana na wadau wa mazingira Tanzania bara na Zanzibar.

Lauwo ataja baadhi ya wadau walioshirikana nao kuandaa mkakati huo kuwa ni Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), na Ofisi Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.


Magogo yaliyokatwa yakisafirishwa.

Anasema moja ya mikakati hiyo ni kuhamasisha upandaji miti nchi nzima kujaza mapengo ya miti iliyopotea, ambayo ina mchango mkubwa katika kusafisha hewa chafu na kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

"Tulianzisha programu ya kupanda miti kitaifa na tunashukuru wadau wengine wa mazingira wanatuunga mkono, mfano hivi karibuni tumepanda miti 500 Sengerema, Kusini mwa Tanzania tumepanda miti takribani milioni 4.5," anasema.

Lauwo anasema, pia wanahakikisha maeneo ya misitu yaliopo nchi kavu na baharini sambamba na maeneo ambayo yana mito na uoto wa misitu hayaharibiwi pamoja na kuboresha mazingira yaliyoathirika.

"Katika hili tunahakikisha tunatoa elimu kwa jamii zinazoishi maeneo yenye uoto wa asili ikiwamo misitu juu ya umuhimu wa kutunza rasilimali hiyo na kuhakikisha zinanyanyuliwa kiuchumi ili siziingie tamaa ya kuvamia na kuharibu.

Anataja shughuli za kiuchumi zinazonufaisha wanakijiji ni biashara ya kuuza hewa ya ukaa, ambapo faida inayopatikana wanagiwa wanakijiji na kuamua kufanya shughuli gani ya maendeleo kama vile kujenga shule na hospitali ili kuboresha maisha yao.

Pia anaitaja biashara ni makubaliano kati ya nchi wanachama wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ulimwenguni kuwa nchi zilizoendelea zitazilipa pesa nchi zinazoendelea kwa kuwa na miti mingi inayonyonya hewa chafu wanayoizalisha kupitia viwanda.

Vilevile wamewapa elimu ya namna wanavyoweza kunufaika na misitu hiyo bila kuiharibu, ikiwamo kufuga nyuki ili wavune asali kwa ajili ya biashara, matunda na dawa zinazopatikana katika rasilimali hiyo hali inayoongeza molari kwa wanavijiji hao kuhifadhi misitu hiyo.

Anasema pia wanashirikiana na vijiji vilivyozungukwa na misitu katika utunzaji huo, baadhi ya vijiji wamevipa umiliki wa rasilimali hiyo na kuwasimamia ili kuhakikisha wanaitunza miti hiyo kwa manufaa ya nchi.

Vilevile walipandisha hadhi ya misitu kutoka misitu ya kawaida hadi kiwango cha juu cha hifadhi ambayo inatumika shughuli za utalii na uhifadhi mazingira hivyo shughuli za kijamii haziruhusiwi zaidi ya hoteli ndogo za miti.

**MENEJA RTI**

Meneja wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Shirika lisilo la kiserikali la RTI ambao ni Mshirika mtekelezaji wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, John Norohna, alisema takwimu zinaonyesha inakadiriwa asilimia 80 ya Watanzania wanategemea maliasili nchi kiuchumi na kijamii.

Alisema kufuatia hali hiyo kuna haja ya kuwekeza nguvu kubwa kwenye kutunza rasilimali hizo ili zisiendelee kuharibika ikiwamo kuja na teknolojia itakayokuwa mbadala ili kuondoa utegemezi wa rasilimali kwa jamii ikiwamo taa na majiko ya sola.

Vilevile alisema jamii zinazoishi kwenye misitu zinahitaji kupewa elimu ya manufaa ya rasilimali hiyo pamoja na kupewa faida inayotokana nayo ili waone umuhimu wa kuitunza, pia elimu ya ujasiriamali kupitia vitu vingine kama vile kutengeneza shanga, kuuza migahawa, mifugo kama njia nyingine ya kujipatia vipato.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utu na Mazingira inayohamasisha upandaji wa miti kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi anasema wanaunga mkono juhudi za serikali za kurudisha uoto wa asili kwa kutoa elimu kuanzia watoto hadi watu wazima kwa mifano ya kupanda miti.

"Tumeanzisha klabu za mazingira katika shule za msingi hapa Dar es Salaam, ambapo tunawafundisha umuhimu wa kuhifadhi mazingira na kupanda miti ili wakue na utaratibu huo na wawe mabalozi wazuri wa mazingira na kuendeleza hiki serikali ilichokianzisha watakapokuwa wakubwa," anasema.

Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), inakadiria kuwa watu milioni 880 duniani kote wanapata angalau sehemu ya mapato na maisha yao kutoka kwa misitu.

Aidha inasema misitu ya kimataifa ina zaidi ya aina 60,000 za miti tofauti na hutoa makazi kwa asilimia 80 ya viumbe vya amfibia, asilimia 75 ya aina ya ndege na 68 za mamalia.

Inaeleza miti pia husaidia kudhibiti mzunguko wa maji na halijoto ya ndani kwa njia ya 'kuvuta pumzi.' Wanafanya hivyo kwa kutia kivuli ardhi na kwa kutoa unyevu kutoka kwa majani yao - mti mmoja unaweza kupitisha mamia ya lita za maji kila siku, na kupoza hewa kama wao.


Sehemu ya msitu wa asili uliopandwa. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

MAZINGIRA

# Atafiti akugundua viumbe kutoweka nchini, atunukiwa udaktari heshima

**Na Beatrice Philemon**

BAADA ya kupata mafunzo ya ukusanyaji, usimamizi na utunzaji taka mijini, pia uhifadhi mazingira kwenye viwanda kutoka Chuo Kikuu cha International Internship (IUU) kilichopo jijini New Delhi India, mtaalamu Dk. Elibahati Kimaro akarejea Tanzania kutumika inavyostahili.

Ni ajenda ya mafunzo inayoendana na Dira ya Maendeleo Endelevu kuelekea mwaka 2030, Dk. Kimaro akiwa na simulizi zaidi kwamba aliporudi nchini mwaka 2019, akaamua kusafiri maeneo mbalimbali ya mkoa wa Kilimanjaro na Manyara kufanya utafiti wa utunzaji viumbe hai na mazingira.

Anautaja ni utafiti uliomsaidia kubaini kuna viumbe hai wameanza kutoweka na wengine wapo hatarini, sasa kunahitajika utafiti zaidi kuangalia mahali kuliko hatarini zaidi, wanyama wanatoweka au wameanza kutoweka, kufanyike mkakati mpya wa kuhifadhi viumbe, kulingana na maeneo wanayoishi.

"Wakati nafanya utafiti niligundua kuwa, kumbe kuna vitu ambavyo vinaweza kupotea duniani, kutokana na hali ya mazingira ya tabia nchi na baadae nilikuja na wazo la kuandika kitabu ambacho kitaonyesha viumbehai ambao wapo hatarini kutoweka duniani, lakini kwa kushirikisha watu mbalimbali," anasema.

Dk. Elibahati Kimaro, anasema utafiti wake katika mkoa Manyara na Kilimanjaro, aligundua kuwapo miti laini inayoweza kupasua miamba na mawe magumu, ikaota na hatimaye kuzalisha msitu.

Anataja utafiti wa Manyara, kwamba kuna aina ya miti wananchi wanaweza kuotesha kwenye maeneo kame, kuwezesha kuwapo uoto wa asili.

Pia, mkoani Kilimanjaro katika kijiji cha Manio, alikokulia anasema kagundua alichokiona miaka ya nyuma, kulikuwapo ndege wengi aina mbalimbali na wanyamapori kama vile mbega na kima.

Anasema, hivi sasa baadhi ya wametoweka mahali hapo. Dk. Kimaro anaendelea: "Wakati nafanya utafiti katika kijiji chetu cha Manio kwanza niliangalia kitu gani kilikuwapo wakati nikiwa mdogo, sasa hivi kuna nini, tofauti ni nini?"

"Hatimaye nikagundua kuwa kuna vitu vingi vimetoweka katika kijiji chetu ikiwamo ndege na wanyamapori," anafafanua.

Hapo ndipo anafafanua dodosa yake kwamba ikamfanya agundue, si kijijini kwao pekee ndio viumbe wametoweka, bali kwingineko zaidi ya Kilimanjaro na Manyara, kuna shida hiyo.



Fundi Sanifu Mwandamizi kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, Dk. Elibahati Kimaro, akionyesha ugunduzi wake, kwenye miti inayopasua miamba. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

**MATOKEO RIPOTI**

Anasema, akatuma matokeo ya utafiti chuoni India alikosoma, ripoti anayoitaja ikawavutia wafadhili wake ambao ni serikali ya India na wakaamua kumfuatilia akiwa nchini Tanzania na mwisho wake wakampatia tuzo ya udaktari wa falsafa wa heshima.

Dk. Kimaro anataja kilichompaisha akagundua miti iliyoweza kupasua miamba na mawe magumu na kuweza kufanya mazingira yakawa mazuri katika eneo hilo katika mkoa wa Manyara.

Hapo mtaaluma huyo anasema, baada ya hapo akaja na wazo la kutengeneza kitabu kinachoonyesha viumbe hai vilivyo hatarini kutoweka duniani, akiwashirikisha wadau mbalimbali.

Ni katika orodha hiyo, anawataja watokao taasisi mbalimbali, wanafunzi vyuo vikuu na vya kati, pia sekondari kutoka nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania.

Rai yake ni kwa Watanzania kutumia fursa za kutafiti au kuandika taarifa za viumbe hai hatarini kutoweka duniani wanakoishi, pia kutoa wazo cha kufanyika, kunusuru na kuhifadhi viumbe hai, sambamba na kurejesha makazi yao endelevu kwa vizazi vijavyo.

"Utafiti huu ni shindano ambalo lipo wazi kwa watu wote ulimwenguni ikiwamo Tanzania, kufanya utafiti. Watu wanaoishi katika maeneo ambayo yapo karibu na misitu, nchi kavu, bahari, maziwa, mito na bonde la ufa wanaweza kushiriki katika shindano hili," anasema.

Shindano hili limeandaliwa na shirika lisilo la kiserikali linalojulikana kama 'Kilimanjaro Field and Class of Environment Protection Initiative (KEPI).

Anasema taarifa zote zitakazopatikana kutoka kwa waliofanya utafiti au kuandika ripoti kulingana na maeneo wanakoishi zitatumika kutengeneza kitabu na kinatarajiwa kusambazwa kwenye taasisi za kimataifa zinazohusika na mazingira.

Lengo, ni kujua yanayotokea duniani ili wachukue hatua za kuhifadhi viumbe hai.

Pia, kitabu kinatarajiwa kusambazwa kwenye taasisi za kitafiti na wadau wengine duniani, kiuzwe na fedha zitakazopatikana, zitatumika kugharamia kupanda miti katika maeneo mbalimbali, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuwalinda viumbe hai.

Anasema, ni shindano la utafiti limenza rasmi Aprili 19 mwaka huu na mwisho wa kuwasilisha Juni 2 mwaka huu, kwa kutumia anwani ya baruapepe: kepi202061@yahoo.com au ellykimaro35@gmail.com

"Tumeamua kuja na shindano hili baada ya kugundua kuwapo mabadiliko ya tabia nchi yamesababisha viumbe hai wengi kupata changamoto ya kuishi na kusababisha changamoto kwenye mimea na wanyama," anasema.

"Ni jukumu letu watu wote ulimwenguni ikiwemo Tanzania kufikiri kuhusu vizazi vijavyo," anasema, akitaja shindano linalosimamiwa na vyombo vya kimataifa, pia waandamizi ngazi ya vyuo vikuu.

# SAFARI 'ZIRO MALARIA' MIKOA TISA IKO 1%

**Na Yasmine Protace**

UGONJWA wa malaria unajulikana kuenezwa na mbu jike, aina ya anopheles. Ni maradhi yanayochangiwa na kuenea viumbe hao, wakihamasishwa na mazingira machafu, hata kusababisha kuwapo na mazalia ya mbu.

Kuna sababu zingine nazo zinatajwa,kuwa kama mazingira ya nyumba yakiwa machafu, yaani kutofyeka majani yaliyozingira nyumba au maji yanayotuama mahali hapo, napo kunachangia kuwapo mazingira ya mbu.

Mapambano kukabili ugonjwa huo, serikali imekuwa ikitoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo, ikiwamo kutoa neti kwa watoto walio na sifa za kupata neti, ikiwamo kwa kina mama wajawazito kupatiwa neti.

Serikali imekuwa ikihamasisha kuwa jamii ifanye usafi wa mazingira lengo ni kujilinda na maambukizi ya ugonjwa wa malaria.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema kwamba, kuna mikoa tisa nchini imefanikiwa kushusha kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa malaria hadi kufikia chini ya asilimia moja, hivyo kufanya asilimia ya watu wanaoishi katika maeneo yenye malaria chini ya asilimia moja kufika 41.

Ni tamko lake waziri huyo, kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani ambayo Kitaifa imeadhimishwa jijini Dar es Salaam.

Waziri Ummy anataja mikoa hiyo ya mafanikio ni: Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Singida, Iringa, Dar es Salaam, Songwe na Mwanza, hata kufanya idadi ya mikoa hiyo kuwa tisa ya sasa, kutoka sita mwaka 2017 yakiwa ni mabadiliko ndani ya miaka sita

"Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya, tunaendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria, kwa kutekeleza afua mbalimbali za kiubunifu katika mapambano dhidi ya malaria na tumeweza kupunguza kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa malaria hadi kufikia chini ya asilimia moja,"anasema.

Hapo anaongeza kuwa, lengo la serikali ni kufikia kiwango cha malaria sifuri, ifikapo mwaka 2030, ila ni kwa mikoa hiyo tisa inayofanya vyema, akio ongeza kuwa, serikali imeweka lengo la 'Ziro Malaria' ifikapo mwaka 2025.

Kuhusu hali ya maambukizi ya ugonjwa huo kitaifa, Waziri Ummy anasema, serikali imepiga hatua kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa huo, hata ikipunguza kiwango cha maambukizi ya ugonjwa kutoka asilimi 14.8 mwaka 2015 na kufikia asilimia 8.1 mpaka sasa.

"Tunaendelea kuwahimiza wananchi kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya endapo watahisi dalili za ugonjwa wa malaria ili kufanya vipimo na kupata tiba sahihi, sio kila homa ni malaria," anasema Waziri Ummy.

Anasisitiza, akiwataka wananchi waendelee kujikinga dhidi ya ugonjwa huo kwa kulala kwenye chandarua na kuweka mazingira safi ili kuangamiza mazalia ya mdudu mbu.



## Makandarasi mradi wa TACTIC kupatikana muda wowote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa kwa sasa serikali kupitia mradi wa uendelezaji miji 45 (TACTIC) ipo kwenye hatua ya kupata makandarasi ambao watajenga barabara za mradi huo nchini.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itajenga kilometa 20 za barabara ya lami zilizopangwa kujengwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba kupitia mradi wa TACTIC.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema kwa sasa mradi huo upo kwenye hatua ya kupata makandarasi wenye uwezo wa kukamilisha mradi huo na muda si mrefu utekelezaji wake utaanza.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqueline Msongozi, alihoji lini barabara ya majengo, Ruvuma, Subira na Muungano itajengwa kwa kiwango cha lami.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi alisema serikali imeshaanza mipango ya ujenzi wa barabara ya Majengo, Ruvuma, Subira na Muungano kwa kiwango cha lami ambapo katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Sh. milioni 517.50 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami nyepesi kilomita moja.

Alisema: "Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kulinga na upatikanaji wa fedha."

**Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kulinga na upatikanaji wa fedha.**

# Ongezeko la vijana wanao 'beti' lawashtua madiwani

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida limeitaka serikali kuchukua hatua za kudhibiti ongezeko la vijana wanaoshiriki michezo ya kubashiri kwa kuwa kunasababisha kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu na ndoa kuvunjika wilayani humo.

Walitoa ushauri huo jana wakati wakijadili kamati ya fedha na uchumi kwenye kikao cha baraza hilo cha robo tatu kuanzia Januari hadi Machi 2023.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Diwani wa Kata ya Mtunduru, Ramadhan Mpaki alisema kwa siku za karibuni kumekuwa na kasi kubwa ya ndoa kuvunjika na uhalifu kuongezeka na sababu kubwa ni kutokana na vijana kujihusisha na michezo ya kubashiri.

Diwani huyo alisema iwapo hakutakuwa na hatua za haraka kudhibiti michezo ya kubashiri ni wazi kuwa hali itazidi kuwa mbaya kwa ndoa kuvunjika na uhalifu kuongezeka.

**Iwapo hakutakuwa na hatua za haraka kudhibiti michezo ya kubashiri ni wazi kuwa hali itazidi kuwa mbaya kwa ndoa kuvunjika na uhalifu kuongezeka.**

Mpaki alitoa ushauri kwa baraza la madiwani kuangalia namna ambayo inaweza kufikisha jambo hili katika mamlaka za kutunga sheria ili ziweze kuona namna ya kulitatua, kwani hali ni mbaya kwa sasa hasa kwa wanandoa.

"Halmashauri yetu iangalie upya sheria ya mchezo huu wa kubashiri, kwani pamoja na kuwa chanzo cha mapato vijana wamekuwa wakicheza mchezo huo hadi usiku wa manane ambapo pia wamekuwa wakipanga vitendo vya kufanya uhalifu ikiwa ni pamoja na kutishia ndoa za watu," alisema na kuungwa mkono na madiwani wenzake.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ally Mwanga, aliwataka watumishi wote na viongozi kuwa wazalendo na kushirikiana ili kuiletea maendeleo wilaya hiyo.

Mwanga alisema suala la ukusanyaji wa mapato ni la kufa na kupona na akasisitiza uzalendo katika jambo hilo na kuwa uhai wa halmashauri yoyote unatokana na mapato na si vinginevyo.

Awali, Ofisa Tawala wa Wilaya hiyo, Dijovson Mtangeki, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, aliipongeza halmashauri hiyo kwa kupata hati safi kwa miaka tisa mfululizo na kuwa mafanikio hayo yametokana na ushirikiano wa kada zote za utumishi wakiwamo madiwani na siasa.

Ofisa huyo alisema halmashauri hiyo imekuwa na miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa fedha na kuwa kazi ya ukaguzi ni lazima ifanywe na viongozi wote na si kumuachia mkuu wa wilaya peke yake.

Alisema licha ya kuwepo kwa kamati, wataalamu, maofisa kata na tarafa kwa ajili ya kusimamia miradi hiyo katika utekelezaji wake madiwani hawawezi kukwepwa kwa namna yoyote ile ukizingatia kuwa miradi mingi inayofanyika ipo kwenye maeneo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Justice Kijazi, alisema mwaka wa fedha wa 2023/ 2024 madiwani wote wa halmashauri hiyo watafanya ziara ya mafunzo kwenda Wilaya ya Tanganyika kujifunza namna bora ya utunzaji wa mazingira kutokana na wilaya hiyo kuwa kinara wa utunzaji mazingira hapa nchini.




Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajab Mabele (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mtambo wa kuzalisha zege na magari yatakayotumika kwenye uzalishaji huo, eneo la Kisasa jijini Dodoma juzi. Wa (pili kushoto) ni Mkurugenzi wa Suma JKT, Kanali Petro Ngata na (wa tatu kushoto) ni Mkuu wa Tawi la Utawala wa Jeshi hilo, Brigedia Jenerali Hassan Mabena. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# JKT yazindua mtambo wa kuzalisha zege

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, amezindua mtambo wa kuzalisha zege huku akiihakikishia serikali kuwa jeshi hilo litakamilisha kwa wakati miradi na kujenga kwa viwango vyenye ubora vinavyotakiwa.

Meja Jenerali Mabele aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizindua mtambo wa kuzalisha zege na magari yatakayotumika kubeba zege ya Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT.

Meja Jenerali Mabele alisema hiyo ni hatua kubwa kwa JKT hasa ukizingatia jeshi hilo likielekea kutimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake, hivyo inaendeleza kazi kwa teknolojia na kuachana na analogia.

"Nashukuru serikali kwa kuendelea kuwa na imani na jeshi hilo kupitia SUMA JKT waendelee kutupatia jukumu la kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ya ujenzi," alisema Meja Jenerali Mabele.

Hata hivyo alisema kitendo cha serikali kuendelea kuwaamini kuwapatia kazi kimewawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na ubora zaidi kwa kutumia zana za kisasa na ndiyo maana wameendelea kupiga hatua kubwa za kununua vifaa cha kisasa ili waendelee kufanya kazi kisayansi zaidi.

Alisema mtambo huo na magari ambayo yamegharimu Sh. bilioni 1.349 vinakwenda kuiwezesha SUMA JKT kuondokana na gharama kubwa walizokuwa wakitumia kununua zege, kukodi magari na kuzisafirisha kwenye miradi yake mbalimbali.

"Mitambo hii itatuingizia fedha kutokana na kuuza zege kwa makandarasi wengine hapa nchini,"alisema Meja Jenerali Mabele.

Alisema huu ni mwanzo lakini uelekeo wao ni kuwa na mitambo ya kisasa kwa wingi zaidi hivyo wataendelea kununua mitambo, ili kuimarisha imani yao kwa serikali kwani watafanya kazi kwa ufanisi zaidi kuliko awali.

Meja Jenerali Mabele, aliwaagiza wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha wanatunza mtambo na magari hayo ikiwa ni pamoja na kuyafanyia matengenezo ya mara kwa mara ili yaweze kudumu na kufanya kazi kwa muda mrefu.

"Mitambo hii katika upya wake itaonekana inafanya kazi vizuri, ili iendelee kufanya kazi kwa ufanisi lazima ninyi mtakaopewa dhamana ya kuisimamia hakikisheni mnaitunza vyema, hili ni agizo kwenu,"alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUMA JKT, Kanali Petro Ngata, alisema ununuzi wa mtambo huo ni moja ya mipango ya shirika hilo ya kununua mitambo ya kisasa katika mwaka wa Fedha 2022/23 huku akiwataka watendaji kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuleta tija na matokeo chanya kwa taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Idara ya Ujenzi SUMA JKT, Mhandisi Morgan Nyoni, alisema mtambo na magari hayo yamegharimu Sh.bilioni 1.349 na utawawezesha kuzalisha zege na kuuza kwenye kampuni zingine zinazofanya kazi za ujenzi hapa nchini.





# Mradi wa kusaidia usimamizi wa mazingira wazinduliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TANZANIA kwa kushirikiana na ubalozi wa Sweden imezindua mradi mpya wa kusaidia usimamizi wa mazingira kwa kuishirikisha jamii ya wenyeji hasa katika kusimamia mfumo ikolojia ujulikanao kwa jina la SUSTAIN Eco.

Mradi huo ulizinduliwa jana jijini Mbeya ambapo wadau mbalimbali walishiriki wakiwamo maofisa kutoka katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na maofisa wa ubalozi wa Sweden.

Washiriki wengine ni wadau kutoka katika mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambayo yanahusika na usimamizi wa mazingira, mashirika yanayotekeleza mradi huo pamoja na wakulima kutoka katika mikoa inayolengwa kunufaika.

Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa na Shirika la Kimataifa la Kulinda Uasilia (IUCN) kwa kushirikiana na mashirika mawili ambayo ni Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) na Shirika la Kulinda Wanyamapori Afrika (AWF).

Mkurugenzi wa Shirika la IUCN, Charles Oluchina, alisema mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la misaada (SIDA) na unatarajiwa kutekelezwa katika mikoa mitatu ambayo ni Morogoro, Rukwa na Katavi.

Alisema shughuli zitakazokuwa zinafanyika ni pamoja na kuwahamasisha

**Tanzania ni miongoni mwa mataifa ambayo yamekuwa yakiathiriwa kwa kiwango kikubwa na uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za kibinadamu.**

wananchi kutumia vizuri rasilimali asili zilizopo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaikumba dunia kwa sasa.

Vilevile alisema watakuwa wanawahamasisha wananchi kufanya shughuli mbalimbali za kiuhifadhi pamoja na kuwafadhili kwenye baadhi ya miradi hiyo ikiwamo ya upandaji miti na ufugaji wa nyuki.

Alisema kwa kuanzia mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu na kwamba serikali ya Sweden imefadhili kwa Dola za Marekani milioni 4.5.

"Mradi huu ni muhimu sana kwa kipindi hiki kutokana na ukweli kwamba mazingira yamekuwa yakiharibiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwamo kukata miti kwa ajili ya kuni na mkaa hali ambayo inasababisha migogoro ya kimazingira," alisema Oluchina.

Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Macias alisema serikali ya nchi hiyo imeamua kufadhili mradi huo ili kuendeleza ushirikiano na Tanzania ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 60.

Alisema kwa sasa kuna baadhi ya viumbe hai muhimu vimeanza kupotea kutokana na uharibifu wa mazingira ambao umekuwa ukifanywa na binadamu ikiwamo viumbe hai vya majini na hata nchi kavu.

Alisema migogoro mingi ya kimazingira imekuwa ikisababishwa na ongezeko kubwa la watu duniani ambalo linasababisha kuongezeka kwa kasi ya uhitaji wa kufyeka miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

"Shughuli hizi za kibinadamu zimekuwa zikisababisha kupotea kwa baadhi ya bioanuai muhimu sana, kwahiyo huu mradi utatusaidia kurejesha mazingira yaliyoharibiwa na sisi tutaendelea kufadhili mradi huu pamoja na miradi mingine kulingana na mahitaji ya serikali," alisema Balozi Charlotta.

Alisema serikali ya Sweden mbali na kusaidia miradi ya maendeleo nchini imekuwa ikisaidia miradi mingine ikiwamo inayohusu masuala ya demokrasia na uhuru wa kujieleza.

Akizindua mradi huo kwa niaba ya serikali, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Mitawe, aliishukuru Serikali ya Sweden kwa kufadhili mradi huo na kuagiza watekelezaji kuhakikisha wanatekeleza vizuri.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa mataifa ambayo yamekuwa yakiathiriwa kwa kiwango kikubwa na uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za kibinadamu.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa kila mwaka Tanzania hupoteza zaidi ya hekta 490,000 za misitu kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwamo kilimo, uchomaji wa mkaa pamoja na kuni.

Alisema ili kukabiliana na matatizo hayo, serikali imeanzisha sera mbalimbali za mazingira pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali kwenye utunzaji wa mazingira.

## Seneti ya vyuo vikuu yajitosa kukisaidia Chuo Kikuu Mzumbe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SENETI ya vyuo vikuu mkoani Mbeya imejitosa kuhamasisha uchangiaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wasichana wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya ili kukabiliana na matatizo ambayo yamekuwa yakiwakumba.

Kwa mujibu wa takwimu kampasi hiyo ina wanafunzi 3,411 ambao kati yao wanawake ni 1,727 na 1,684 lakini hosteli zilizopo zinatosha wanafunzi 410.

Katibu wa Seneti ya Vyuo Vikuu Mkoa wa Mbeya, Issa Mwazembe, alisema uongozi wa chuo hicho umeanzisha mchakato wa kujenga hosteli zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi wa kike 800 na itagharimu zaidi ya Sh. bilioni tano.

Alisema wameamua kushiriki kwenye uhamasishaji wa wadau ili waharakishe ujenzi wa mabweni hayo na kuwapunguzia wasichana wanaosoma kwenye chuo hicho adha ambazo wamekuwa wakikumbana nazo.

Alisema chuo hicho kinachukua wanafunzi wanaosoma ngazi ya cheti mpaka shahada ya uzamivu lakini wanaopata tatizo zaidi ni wale wanaosoma ngazi ya cheti.



Mnufaika wa Mradi wa Dreams chini ya ufadhili wa mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani PEPFAR, Neema Mwakyusa, akionyesha namna mafunzo ya ufundi yalivyomwezesha kupata ujuzi wa kushona ili kujipatia kipato kwa maofisa wa Ubalozi wa Marekani nchini, walipotembelea Kata ya Igurusi wilayani Mbarali mkoani Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wasichana 80,000 wanufaika na mradi wa Dreams

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WASICHANA 80,000, wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 24 kutoka katika halmashauri tatu za Mkoa wa Mbeya, wamenufaika na mradi wa Dreams wenye lengo la kuwasaidia wasichana walio katika umri wa rika balehe kuepukana na mazingira hatarishi ya kuambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani, PEPFAR kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania unaadhimisha miaka 20 ya mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU ambapo ufadhili huo kupitia PEPFAR na mashirika ya WRAIR-DOD na HJFMRI umepata mafanikio makubwa mkoani Mbeya.

Mratibu wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Petro, alisema hadi sasa wasichana 80,000 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Mbarali na Jiji la Mbeya wameondoka kwenye mazingira hatarishi ya kupata maambukizi ya Ukimwi kupitia mradi wa Dreams.

Aliongeza kuwa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu ya VVU kata 89 za halmashauri tatu zinazotekeleza mradi huo zimefikiwa na vituo 47 vya afya vinavyotoa huduma zote muhimu ikiwamo utoaji wa dawa za kufubaza maambukizi ya VVU, tiba ya magonjwa ya ngono, elimu ya matumizi ya kondomu ili kuepukana na maambukizi mapya.

Alisema hadi sasa watoa huduma 200 wamejengewa uwezo wa namna bora ya kutoa huduma za matibabu na kutoa rufani za kuwaunganisha na huduma za kiuchumi pamoja na kupatiwa bima ya afya iliyoboreshwa ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Mshauri wa Kinga za UKIMWI wa Shirika la WRAIR-DOD ya ubalozi wa Marekani, Dk. Alick Kayange, alisema miongoni mwa mafanikio wanayojivunia katika mapambano ya maambukizi ya VVU ni upatikanaji wa vifaa tiba kote nchini pamoja na mafunzo kwa watoa huduma ngazi zote.

Alisema kwa sasa dawa za kufubaza makali ya VVU zinapatikana kote nchini lakini pia PEPFAR wameweka maabara za kisasa za ufuatiliaji wa magonjwa yatokanayo na ugonjwa huo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Kwangura Missana, alisema mradi wa dream umewasaidia vijana wa kike kuepukana na makundi hatarishi ambayo yanasababisha maambukizi ya UKIMWI.



# Uwekaji anwani za makazi wafanikiwa asilimia 80

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema kazi ya uwekezaji wa anwani za makazi imefanikiwa kwa asilimia 80 na kwa sasa matatizo yote yaliyojitokeza yanafanyiwa kazi ili kufanikisha kukamilisha kwa ufanisi.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hamza Hassan Juma, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Viti Maalumu, Fatuma Ramadhan Mandoba, aliyetaka kujua kazi ya uwekaji wa anwani za makazi limefanikiwa kwa kiasi gani.

Juma alisema kazi hiyo inaendelea, kwamba wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wanaendelea kufanya uhakiki maalumu ili kupata usahihi wa anwani zilizowekwa katika kipindi cha operesheni.

Alisema hadi sasa wilaya tisa za Zanzibar zimefikiwa na kuhakikiwa ikiwamo Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Kaskazini Unguja, Kusini Unguja pamoja na wilaya za Pemba.

Waziri huyo alisema anwani 528,417 zimesajiliwa katika mfumo wa kielektroniki.

Aidha, alisema tayari nyumba hizo zimepatiwa alama za utambulisho hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa mji wenye mipango na utambulisho wake katika masuala ya anwani za makazi.

Alisema kazi ya kuweka alama za vibati katika nyumba za wananchi kwa ajili ya utambuzi linaendelea ambalo litasaidia na kurahisisha mawasiliano ya kuzitambua shehia husika.

**Tayari nyumba hizo zimepatiwa alama za utambulisho hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa mji wenye mipango na utambulisho wake katika masuala ya anwani za makazi.**

# Mradi wa kuendeleza kilimo, uvuvi kuleta neema

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI zaidi ya 200,000 wanatarajiwa kunufaika na mradi wa kuendeleza maendeleo ya kilimo na uvuvi Zanzibar, ambao unatekelezwa na Shirika la Kimataifa la Kuimarisha Kilimo, Ufugaji na Uvuvi (IFAD).

Mradi huo wa muda wa miaka sita ulioanza kutekelezwa mwaka 2021, utafanya kazi katika pande mbili za muungano kwa baadhi ya mikoa ikiwamo, Morogoro, Manyara, Singida, Dodoma, Tabora, Mwanza, Shinyanga, Geita, Pwani, Lindi na mikoa yote ya Zanzibar.

Akizungumza wakati akiongoza kikao cha majumuisho kwa wajumbe wa mradi huo, Mkurugenzi wa Sera na Uratibu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Paul Sangawe, alisema mradi huo utawawezesha wakulima wa mwani kulima kilimo cha kisasa ili kupata tija na kuondokana na kilimo cha mazoea ambacho uzalishaji wake ni mdogo.

Mkurugenzi huyo alisema mradi huo utabadilisha kilimo cha mwani Zanzibar na kuongeza mnyororo wa thamani wa zao hilo ambalo asilimia 90 linalimwa na wanawake.

Kuhusu kuwanufaisha wavuvi, alisema mradi huo utanunua boti nane za uvuvi wa bahari kuu ili kuimarisha maisha ya wavuvi kwa Zanzibar na Tanzania Bara.

**Lengo letu la kufika hapa Zanzibar ni kuangalia utekelezaji wa mradi huu kwa vile tayari umeshafika mwaka wa pili tangu kuanza kufanyakazi na kwa sasa unaendelea vizuri.**

Alisema ununuzi wa boti hizo unatarajiwa kukamilika katika kipindi kifupi kijacho na tayari watu wa mazingira wameshafanya uchunguzi na kubaini kuwa hakutakuwa na athari za kimazingira katika kuendeleza mradi huo.

Alisema gharama za mradi huo hadi kukamilika kwake ni Dola za Marekani milioni 58.8 kutoka Shirika la IFAD la Marekani.

"Lengo letu la kufika hapa Zanzibar ni kuangalia utekelezaji wa mradi huu kwa vile tayari umeshafika mwaka wa pili tangu kuanza kufanyakazi na kwa sasa unaendelea vizuri," alisema.

Mratibu wa mradi huo kwa upande wa Zanzibar, Amina Ussi Khamis, alisema kwa upande wa Zanzibar mradi utawanufaisha zaidi vijana na wanawake hasa wakulima wa mwani kwa kulima kisasa na kuongeza tija wa zao hilo.

Alisema vijana watanufaika kupitia sekta ya uvuvi na kuvua samaki katika bahari kuu ili kupata samaki wengi zaidi na kuongeza kipato chao.

Alisema licha ya kuonekana kuwa sekta ya uvuvi imetawaliwa na wanaume lakini hivi sasa hata wanawake wamejikita katika sekta hiyo hivyo wakiwezeshwa kwa kupatiwa zana za kisasa watahamasika zaidi.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, amewaomba wajumbe hao kujadili kwa kina na kufikia mazimio ya ziara hiyo kwa manufaa ya Tanzania.

Alisema miongoni mwa malengo ya wizara hiyo ni kuona wananchi wananufaika na kilimo cha mazao ya baharini ili kukuza kipato chao.

Aidha alisema serikali imeanzisha wizara hiyo ili wananchi kunufaika kiuchumi hasa vijana kupata ajira kupitia sekta ya uvuvi.

Hata hivyo alisema kwa kuthamini wakulima wa mwani serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mwani eneo la Camanangwe kisiwani Pemba ili kuongeza thamani ya zao hilo.




Mkurugenzi wa Asma Mwinyi Foundation (AMF), Asma Mwinyi (wa pili kushoto), akishirikiana na wawakilishi wa kampuni ya ASAS, kukabidhi msaada wa jokofu moja, mzani wa kupimia uzito mmoja na maziwa ya mtindi paketi 450 kwa wagonjwa wa Hospitali ya Mnazi Mmoja jijini Zanzibar juzi, ikiwa ni juhudi za kuunga mkono Mkutano Mkuu wa Asasi za Kiraia Zanzibar (ZANGOF). **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Sheria ya Rushwa, Uhujumu Uchumi kufumuliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema serikali inatarajia kuwasilisha marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ili iendane na wakati, kudhibiti matukio ya rushwa.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya serikali katika kuviwezesha vyombo vya kutoa haki na maamuzi kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa mujibu wa sheria.

Alisema sheria hiyo itafanyiwa marekebisho makubwa kwa lengo la kuiwezesha ZAECA kutekeleza majukumu yake katika mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema rushwa ni adui wa haki na Serikali ya Zanzibar imeweka kipaumbele katika mapambano ya rushwa ili kutokomeza katika maeneo mbalimbali ikiwamo katika taasisi za serikali.

Waziri huyo alisema ZAECA tayari imeipitia miradi yote ya UVIKO -19 kuona kwa kiasi gani fedha halali zimetumika katika utekelezaji ikiwamo ujenzi wa hospitali za wilaya 11 pamoja na shule za msingi na sekondari.

Aidha alisema Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imepiga hatua kubwa katika kufanya mahesabu ya serikali na kufichua ubadhirifu katika matumizi mabaya ya fedha za umma.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ALLY BARUANI MACHO** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 348 DBU, MC 833 BDM, MC 348 DCN** zote aina ya **TVS KING.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**DAR/KIG/21570/2023.**

## IN THE DISTRICT COUTR OF DODOMA AT DODOMA

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.59 OF2023**

**In the matter of the Estate of the NOAH DAVID MASAULWA**

**And**

**In the matter of an Application for letters of Administration by RAHEL ASHERY SEMU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before 26th Day of 6,2023

**Dated at Dodoma this 16th day of May 2023**

PETITIONER

**Presented for filling this 24th Day of 5,2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEORGE WILBERT DIMALE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S1197-0145** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **GREEN ACRES SEKONDARI** mwaka **2008.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DAR/URA/RB/176192/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIANA KOSHUMA MWINGIRA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 487 DEB – TOYOTA HARRIER** yenye Chassis No. **ACUB00009185. ENGINE No. 2AZ0321541.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**KW/RB/2305/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **JABIRI ABDALLAH TEKELO** anatangaza kupotea na kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 859 CVL.**

Yenye Chassis Namba:

**JOBXKG609828**

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Polisi:

**DAR/PHQ/RB/175065/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **JABIRI ABDALLAH TEKELO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 694 CLP.**

Yenye Chassis Namba:

**DAPJOB4KG09114**

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Polisi:

**DAR/PHQ/RB/175067/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JAMES MWITA IKWABE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba ya usajili **MC 527 DTX - TVS KING.** Chassis namba **MD6M14PA9P4A04633.** Engine namba **AK4AP4804708.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**DAR/CEN/RB/176941/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JANETH ANTIDIUS MWOSHEZI** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index **NO. S0731/0037 Mwaka 2020** Shule ya Sekondari Makongo ,kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa .Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa polisi: DOD/DOD/RB/163092/2023.**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Malema, nitaipatia Russia silaha

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

KIONGOZI wa Chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) cha Afrika Kusini, Julius Malema, amesema ataipatia silaha Russia kwa sababu taifa hilo liko katika vita vya kupinga ubeberu.

Malema aliiambia BBC jana kuwa Afrika Kusini ni mshirika wa Russia na kwamba msimamo wa serikali ya ANC wa kutojihusisha na siasa unahusu vita vya Ukraine pekee.

"Nitaenda zaidi ya urafiki na Russia katika vita, nitaungana nayo na nitasambaza silaha," alisema Malema.

Aliongeza kuwa EFF pia inataka Afrika Kusini kujiondoa katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC).

Awali ICC ilitoa hati ya kukamatwa kwa Rais wa Russia, Vladimir Putin, kwa madai ya uhalifu wa kivita, huku Malema akiahidi kuzuia jaribio lolote la kumkamata mhasimu huyo wa Ukraine iwapo atahudhuria mkutano wa kilele wa Brics unaotarajiwa kufanyika Juni mwaka huu mjini Cape Town.

Wito wa Malema unakuja wakati huu kukiwa na mzozo wa kidiplomasia baada ya balozi wa Marekani nchini Afrika Kusini alipodai kuwa silaha na risasi zilipakiwa kwenye meli ya Russia iliyotia nanga nchini humo Desemba 2022, kitendo kilichokanushwa vikali na serikali ya Afrika Kusini.

*RFI*

# IMF kuipatia Kenya mkopo dola bil. 1

**NAIROBI, Kenya**

SHIRIKA la Fedha la Kimataifa (IMF) na Kenya wamefikia makubaliano ambayo yanaweza kufungua ufadhili mpya wa dola bilioni moja, zaidi ya Sh. trilioni 2.3 ambayo huenda ikapunguza shinikizo la kifedha katika taifa hilo.

Kenya imekuwa ikikabiliwa na matatizo ya kifedha kutokana na kuongezeka kwa viwango vya riba ya mikopo ya kimataifa na athari za ukame mbaya zaidi katika miongo minne, ingawa mkurugenzi mkuu wa IMF, alisema kwamba hatarajii kuwa nchi hiyo itashindwa kulipa madeni yake.

IMF ilisema katika taarifa yake kwamba mikataba hiyo ilijumuisha ukaguzi uliofanyika siku za karibuni ukiwa ni wa mpango wa ukopeshaji wa ziada, na mipango ya usaidizi wa kulipa mikopo, iliyoidhinishwa mwezi Aprili mwaka 2021 katika mpango mpya chini ya mfumo wa ustahimilivu na uendelevu.

Pia ilibainishwa kuwa IMF ilikubaliana na maofisa wa Kenya kuongeza muda wa mpango wa upanuzi na usaidizi wa kuongeza mikopo kwa muda wa miezi 10, hadi mwezi Aprili mwaka 2025 ili kutoa muda zaidi wa kutimiza masharti yote, na kuongeza kiasi cha pesa kinachopatikana kwa Kenya chini ya mkopo huo, kwa takriban dola milioni 544.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Kenya pia itapata takriban dola milioni 544 chini ya mpango wa ustahimilivu na uendelevu, ulioanzishwa katika juhudi za kuimarisha ustahimilivu na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Vile vile, IMF ilisema ufadhili wa jumla uliotolewa kwa Kenya chini ya mpango huo wa mkopo ulifikia takriban dola bilioni 3.5, na kwamba makubaliano ya kiwango cha wafanyakazi yanatarajiwa kujadiliwa na bodi yake kuu, mwezi Julai mwaka huu.

*VOA*



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy, akiwa pamoja na wanajeshi wa taifa hilo walioko mstari wa mbele katika vita, baada ya kuwatembelea, kwenye maeneo ambayo hayakubainishwa. **PICHA: MTANDAO**

# Nchi 3 zaongoza ukoloni mamboleo

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

MATAIFA matatu yakiongozwa na Korea Kaskazini, Eritrea na Mauritania zimetajwa kuongoza katika kukithiri kwa utumwa mamboleo ulimwenguni, kwa kuwaozesha na kuwafanyisha watu kazi kwa kuwalazimisha.

Hayo yalibainishwa jana katika ripoti ya mwaka huu iliyotayarishwa na shirika la hisani la haki za binadamu la Walk Free, ikibainishwa kwamba hali ya ukoloni mamboleo imekuwa mbaya zaidi kuliko miaka mitano iliyopita.

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa watu milioni 50 waliishi katika mazingira ya utumwa mamboleo mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la watu milioni 10 kutoka mwaka 2016, wakati tatizo hilo lilipopimwa kwa mara ya mwisho.

"Idadi hiyo inajumuisha watu milioni 28 wanaofanyishwa kazi kwa kulazimishwa na milioni 22 wanaoishi katika ndoa za kulazimishwa," ilisema.

Uchunguzi huo ulisema kuwa hali inazidi kuwa mbaya zaidi wakati kukishuhudiwa ongezeko la mizozo ya kivita, uharibifu mkubwa wa kimazingira na athari za janga la virusi vya corona, miongoni mwa sababu nyingine.

Ripoti inafafanua utumwa wa kisasa kama unaojumuisha kazi na ndoa za kulazimishwa, utumwa wa madeni, biashara ya kulazimishwa ya ngono, usafirishaji haramu wa binadamu, vitendo vinavyofanana na utumwa na uuzaji wa watoto na kuwatumia vibaya.

"Msingi muhimu wa utumwa unahusu kuondolewa kimfumo kwa uhuru wa mtu kutoka haki ya kukubali au kukataa kazi hadi uhuru wa kuamua kama lini na nani wa kufunga naye ndoa," ilifafanua.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kwa kuzingatia kigezo hicho, Korea Kaskazini ndiyo ina kiwango kikubwa cha kuenea kwa utumwa wa kisasa na kwamba watu 104.6 kati ya 1,000 wako katika tatizo hilo. Ikifuatiwa na Eritrea 90.3 na Mauritania 32, ambayo mwaka 1981 ilikuwa nchi ya mwisho duniani kuharamisha utumwa wa kurithi.

Aidha, ilibainisha kuwa nchi 10 zenye utumwa mamboleo uliokithiri zina sifa zinazofanana, ikiwamo ulinzi mdogo wa uhuru wa raia na haki za binaadamu na kwamba nyingi ziko katika maeneo yanayokumbwa na mizozo, ukosefu wa utulivu wa kisiasa, au ni kitovu cha idadi kubwa ya watu wanaoishi katika mazingira magumu kama wakimbizi au wafanyakazi wahamiaji.

Hata hivyo, ilisema katika nafasi 10 za kwanza ulimwenguni ni Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu na Kuwait, ambako haki za wafanyakazi wahamiaji zinadhibitiwa na mfumo wa ufadhili wa 'kafala'.

Ilibainisha kuwa nchi nyingine katika 10 bora ni Uturuki, ambayo inawahifadhi mamilioni ya wakimbizi kutoka Syria, Tajikistan, Russia na Afghanistan.

Vile vile, ripoti inasema wakati kazi za kulazimishwa ni kitu cha kawaida katika nchi za kipato cha chini, inaunganishwa pakubwa na mahitaji ya nchi za kipato cha juu.

Ripoti hiyo inasema nchi za G20 zinazoundwa na Umoja wa Ulaya na madola 19 makubwa kiuchumi kwa sasa zinaagiza bidhaa za thamani ya dola bilioni 468 ambazo zipo katika hatari ya kuzalishwa kwa nguvu kazi ya kulazimishwa, kutoka dola bilioni 354 katika ripoti ya awali.

Bidhaa za kielektroniki zinasalia kuwa zenye thamani ya juu zilizo hatarini, zikifuatiwa na nguo, mafuta ya mawese na paneli za jua, ikiwa ni dalili ya kuwapo na mahitaji makubwa ya bidhaa za nishati mbadala.

*DW*

# POLISI TANZANIA YAZITISHA SIMBA, AZAM LALA SALAMA

**Na Hadija Mngwai**

HUKU ikiwa katika hatari ya kushuka daraja, Polisi Tanzania imesema itapambana kwa 'jasho na damu' kuhakikisha inavuna pointi sita katika mechi zake mbili zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Polisi Tanzania imebakisha mechi mbili zote za ugenini ambazo ni dhidi ya Simba na Azam FC, zote za Dar es Salaam.

Maafande hao wako katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara mkononi wana pointi 25, wakiwa mbele ya Ruvu Shooting yenye pointi 20 ambayo inaburuza mkia na rasmi imeshashuka daraja.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Polisi Tanzania, Frank Lukwalo, alisema timu yao haijakata tamaa na imejipanga kuonyesha soka la burudani katika mechi zilizobakia ili malengo yao ya kupata ushindi yatimie.

Lukwalo alisema wachezaji wao watacheza kwa tahadhari kwa sababu wanahitaji kupata ushindi katika mechi zao bila kujali matokeo ya michezo mingine yatakavyokuwa.

"Tumejipanga kutumia kauli mbiu yetu ya machozi, jasho na damu, ili kuhakikisha tunavuna alama sita zitakazotuwezesha kubaki katika Ligi Kuu Bara.

Mwalimu Zahera (Mwinyi), anaendelea na mikakati yake ya kukisuka vyema kikosi ili tupate ushindi kwenye mechi zetu mbili zilizobakia dhidi ya Simba na Azam FC. Mikakati bado inaenda vizuri katika mechi hizi zilizobakia tufanye vizuri, hatujakata tamaa hadi sasa na hakuna mchezaji yoyote aliyekata tamaa hadi mwisho wa ligi, hali ya kikosi ipo vizuri kuelekea michezo hiyo," alisema Lukwalo.

Aliongeza wanataka kuonyesha kandanda safi kama walivyofanya katika mechi dhidi ya Ihefu na Mtibwa Sugar ambayo walipata ushindi.

Yanga tayari imeshatangazwa mabingwa wa msimu huu wa 2022/2023 kutokana na kufikisha pointi 74, ambazo hazifikiwi na timu nyingine.



Kocha wa ngumi wa Urafiki Boxing Academy, Akaroly Godfrey (wa pili kushoto), akiwa katika mazoezi na mabondia chipukizi wa kituo hicho kilichoko Urafiki, Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Simba Queens yauota ubingwa

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuvuliwa ubingwa, benchi la ufundi la Simba Queens, limesema linajipanga upya kuhakikisha msimu ujao linarudisha kombe lao Ligi Kuu ya Wanawake mikononi mwao.

Simba Queens ambayo ilifanya vyema pia katika mashindano ya kimataifa msimu uliopita, imevuliwa ubingwa na JKT Queens kwa tofauti ya pointi moja.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, alisema amesikitika kuona timu yake imepoteza ubingwa msimu huu lakini amekiri ligi ilikuwa na ushindani mkubwa. Lukula alisema licha ya kukosa ubingwa anawapongeza wachezaji wake kwa kufanya vizuri na kuongoza kufunga idadi kubwa ya magoli.

"Ingawa hatujapata ubingwa msimu huu lakini timu yangu haijafanya vibaya, sisi ndio tumefunga idadi kubwa ya magoli kuliko timu nyingine, tunaanza kujipanga kwa ajili ya msimu ujao," alisema Lukula.

Kocha huyo alisema atayafanyika kazi mapema mapungufu madogo madogo yaliyojitokeza katika michezo waliyoicheza ili kurejea msimu mpya wakiwa na nguvu zaidi.

"Kuna makosa madogo madogo yaliofanyika katika safu ya ushambuliaji, nitayafanyia kazi mara tu ratiba itakapotoka ili kuanza maandalizi ya msimu ujao mapema," alisema kocha huyo.

## MeridianBet yaja na Aviotor Kasino

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya mchezo wa kubashiri ya Meridianbet Tanzania imekuja na promosheni ya kijanja kwa mchezaji anapocheza Aviator kasino ya mtandaoni wanakupatia bashiri 20 za bure ili kuongeza ushindi.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet Tanzania, Martin Nkurlu, alisema Kasino ya mtandaoni ya kampuni hiyo inaendelea kuwajali wateja kwa kuwapatia bonasi, ofa na promosheni za kijanja.

Nkurlu alisema promosheni hiyo inachezwa kwa aina ya safari ya kurusha ndege ya Aviator na huanza pale mchezaji anapoweka dau lake katika sehemu mbili ya kulia na kushoto.

"Kama unataka ushindi mkubwa unatakiwa usubiri ndege iruke, kadri inavyopaa angani ndio ushindi unavyoongezeka, hiyo haitoshi Meridianbet kasino ya mtandaoni wameamua kuongeza mzuka kwenye mchezo huo kwa kutoa 'mvua 20' za bure kwa wachezaji 10 wanaocheza zaidi mchezo huu," alisema Nkurlu.

Aliongeza promosheni "Aviator Bonanza, beti kibao za bure" iliyoanza Mei 19 itamalizika Mei 31, mwaka huu na inapatikana kwa wateja wote wa Meridianbet.

## Mtibwa Sugar SC kumwaga 'mboga'

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mtibwa Sugar inatarajia kutoa msimamo wake kutokana na timu hiyo kuwa na matokeo ya kusuasua kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara miaka ya hivi karibuni, imeelezwa.

Mtibwa Sugar imebakiza mechi mbili dhidi ya Kagera Sugar na Geita Gold na zote watacheza nyumbani kwao Manungu Complex.

Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, amesema, klabu hiyo inatarajia kuweka wazi kilichowaangusha katika misimu miwili mfululizo na kuishia kupambana kujinusuru na janga la kushuka daraja.

"Kwanza niwatoe wasiwasi Watanzania Mtibwa Sugar hatushuki daraja, naamini tunashinda mechi mbili tulizosaliwa, ila timu yetu tangu ipande daraja mwaka 1995 na kuanza kucheza Ligi Kuu, misimu hii miwili imekuwa mibaya sana kwetu," alisema Kifaru.

Aliongeza Mtibwa Sugar yenye pointi 29 na iko katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi hiyo ni timu inayotakiwa kuwania au kupigania mataji na si kupambana kujinusuru kuondoka mkiani.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUUZA NANE
ARSENAL iko tayari kuuza wachezaji nane wa kikosi cha kwanza msimu huu, huku kiungo wa kati wa Leicester City na England, James Maddison, mwenye umri wa-miaka 26 na kiungo wa kati wa West Ham, Declan Rice (24) wakiwa miongoni mwa wachezaji wapya wanaotaka kuwasajili. ***(Mirror)***

### GUNDEGAN ANUKIA ARSENAL
KLABU ya Arsenal imeonyesha nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, ikiwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 hatakubali mkataba kusaini mpya na Manchester City. ***(ESPN)***

### ANDY ANUKIA MADRID
REAL Madrid wamemwongeza nyota wa Liverpool na nahodha wa Scotland, Andy Robertson, mwenye umri wa miaka 29 kwenye orodha ya wachezaji wanaowawinda ili kuchukua nafasi ya beki wa Ufaransa, Ferland Mendy, mwenye miaka 27. ***(Mail)***

### ALVAREZ ATAJWA BAYERN
KLABU ya Bayern Munich imemtambua mshambuliaji wa Manchester City na Argentina, Julian Alvarez, mwenye umri wa miaka 23 kama mlengwa wa uhamisho wa majira ya joto. ***(Bild)***

### UNITED YAMTAKA KANE
MANCHESTER United inafikiria kuwasajili washambuliaji wawili wapya, lakini wanaweza wasiafikiane na Tottenham Hotspur kuhusiana na usajili wa nahodha wa England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29. ***(90min)***

### KUDUS KUONDOKA AJAX
MSHAMBULIAJI wa Ajax, Mghana Mohammed Kudus, ambaye anahusishwa na Arsenal, Manchester United na Newcastle United, amekataa kuongeza mkataba katika klabu hiyo na wakala wake anaamini "sasa ni wakati muafaka" kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuondoka. ***(De Telegraaf)***

### ONANA KUIBEBA EVERTON
KLABU ya Everton inapanga kumuuza kiungo wa kati wa Ubelgiji, Amadou Onana, mwenye umri wa miaka 21 kwa pauni milioni 60 ili kufadhili mipango yao ya uhamisho wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### KOUNDE KUONDOKA BARCA
BEKI wa Ufaransa, Jules Kounde, ameiambia Barcelona anataka kuondoka katika klabu hiyo katika msimu wa joto, hata hivyo timu hiyo ya LaLiga itazingatia tu ofa za euro milioni 80 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Sport)***

### RONALDO KUREJEA ULAYA
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, tayari anataka kuondoka katika klabu ya Al Nassr ya Saudi Arabia na huenda akarejea Ulaya. ***(Mundo Deportivo)***

### JUVE: VLAHOVIC HAUZWI
JUVENTUS imesema haina nia ya kumuuza mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic (23) baada ya kukatwa pointi katika hatua ambayo huenda ikaifanya klabu hiyo kukosa nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(90 Min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SAKA AMALIZANA NA ARSENAL HADI 2027

Mshambuliaji huyo asema anaamini atafikia malengo akiwa hapo na...

**LONDON, England**

BUKAYO Saka ametia saini mkataba mpya wa kubakia Arsenal hadi mwaka 2027, akisema klabu hiyo "ndipo sehemu sahihi ya kupiga hatua inayofuata".

Mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya England amefunga mabao 14 kwa Washikabunduki hao msimu huu, na kutoa pasi 11 za mabao.

Akiwa na umri wa miaka 21 tu, tayari ameichezea klabu hiyo mechi 178 na ameshiriki katika mechi zote za Ligi Kuu England katika kipindi cha mismu miwili iliyopita.

"Nimefurahi sana tu," alisema Saka.

"Kumekuwa na mazungumzo mengi na muda umepita, lakini niko hapa sasa. Nadhani hii ni klabu sahihi, mahali pazuri kupiga hatua inayofuata. Ni klabu nzuri, angalia tulipo.

"Kwangu mimi, ni juu ya kufikia malengo yangu binafsi - kiasi gani ninajisukuma na kudai kutoka kwangu kila mchezo, wiki baada ya wiki.

"Halafu nina watu wote wanaofaa karibu nami katika suala la familia, na ninapokuja kwenye mafunzo, wachezaji wenzangu na wafanyakazi wananipa ushirikiano mkubwa.

"Nadhani nina kila kitu ninachohitaji ili niwe mchezaji bora zaidi, ninaweza kuwa, na ndiyo sababu nina furaha kubaki hapa na kuwa hapa kwa siku zijazo, kwa sababu ninaamini tunaweza kufikia mambo makubwa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,117,4
MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
CHELSEA
1 | 1.63
X | 3.89
2 | 4.55
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PSG : NEYMAR HANA NIA YA KUTUA UNITED



**PARIS, Ufaransa**

WINGA wa PSG, Neymar Jr ambaye anahusishwa na tetesi za kujiunga na Manchester United, imethibitika taarifa hizo sio kweli kama ambavyo zilizuka siku mbili zilizopita.

Neymar Jr ambaye amekuwa na majeraha kwa miezi kadhaa ndani ya PSG alihusishwa na kujiunga na United, lakini kwa mujibu wa taarifa ya klabu yake iliyonukuliwa na ESPN imesema hakuna majadiliano yeyote baina ya mchezaji huyo na wababe hao wa soka wa pale kwenye dimba la Old Trafford.

Winga huyo wa kimataifa wa Brazil inaelezwa hana furaha ndani ya miamba ya soka wa Ufaransa, jambo ambalo linaelezwa afikirie kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Taarifa kwa mujibu wa ripoti hiyo, hata kama Neymar ataondoka PSG, lakini hakuna mpango wowote uliowazi atatua Manchester United.

Taarifa kutoka PSG zinaeleza klabu hiyo inafanya mazungumzo kwa ajili ya kuachana na Neymar Jr kwenye dirisha kubwa lijalo majira ya joto, kwa sababu haipendezwi na mwenendo wa mchezaji huyo.

Mapema mwezi uliopita mashabiki wa PSG walikusanyika nje ya nyumba ya Neymar na kumtaka aondoke kwenye klabu yao.

# Robertson atakiwa Real Madrid

**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa Liverpool, Andy Robertson, ameripotiwa kuingia kwenye rada za kutakiwa na Real Madrid katika dirisha hili la majira ya joto.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, nahodha huyo wa Scotland mwenye umri wa miaka 29 anatazamwa na klabu hiyo ya Ligi Kuu Hispania kama mbadala wa beki anayesumbuliwa na majeraha, Ferland Mendy.

Hata hivyo, Robertson amepewa mkataba na Liverpool hadi mwaka 2026 na hajaonyesha nia ya kuondoka.

Wakati huo huo, gazeti la Daily Mirror linaripoti Arsenal wako tayari kuhama milima ili kuongeza mtaji wao wa uhamisho.

Gazeti hilo limesema Real Madrid inaona safu yake ya ulinzi inaweza kulegalega endapo wasipoongeza mlinzi mwingine kwa ajili ya msimu ujao.

Madrid msimu huu umekuwa mbaya kwao wakiwa wametwaa taji moja tu la Copa Del Rey, huku wakishindwa kutete taji lao la Ligi Kuu lililochukuliwa na wapinzani wao, Barcelona pia akiwa bingwa mtetezi alitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya nusu fainali na Manchester City.



17,539/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/05/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs AS Roma | 2.40 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 27/05/23 | 20:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 2.80 | 3.40 | 2.29 |
| 03. 27/05/23 | 22:00 | Montpellier HSC vs OGC Nice | 2.47 | 3.30 | 2.60 |
| 04. 28/05/23 | 02:30 | Orlando City SC vs Atlanta United FC | 2.15 | 3.10 | 2.85 |
| 05. 28/05/23 | 15:30 | Carlisle United vs Stockport County FC | 3.00 | 3.15 | 2.28 |
| 06. 28/05/23 | 15:30 | AZ Alkmaar vs PSV Eindhoven | 2.55 | 3.50 | 2.40 |
| 07. 28/05/23 | 15:30 | Fortuna Sittard vs NEC Nijmegen | 2.50 | 3.40 | 2.50 |
| 08. 28/05/23 | 16:00 | AC Monza vs US Lecce | 2.70 | 3.10 | 2.50 |
| 09. 28/05/23 | 17:15 | Racing Santander vs FC Cartagena | 2.55 | 3.05 | 2.65 |
| 10. 28/05/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Newcastle United | 2.80 | 3.35 | 2.29 |
| 11. 28/05/23 | 18:30 | Aston Villa vs Brighton & Hove Albion | 2.16 | 3.55 | 2.90 |
| 12. 28/05/23 | 18:30 | Leeds United vs Tottenham Hotspur | 2.65 | 3.45 | 2.34 |
| 13. 28/05/23 | 20:00 | Cadiz CF vs RC Celta de Vigo | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 14. 28/05/23 | 20:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 15. 28/05/23 | 20:00 | Girona FC vs Real Betis Seville | 2.60 | 3.15 | 2.60 |
| 16. 28/05/23 | 21:45 | Juventus Turin vs AC Milan | 2.26 | 3.25 | 2.95 |
| 17. 28/05/23 | 22:00 | SC Corinthians SP vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.05 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 25/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1356 | Binh Phuoc vs QNK Quang Nam | 3.03 | 3.13 | 2.17 |
| 13:00 | 1967 | BA Ria Vung Tau FC vs Binh Thuan | 1.52 | 3.79 | 5.33 |
| 13:00 | 3575 | FC Minaj vs Rukh Vinnyky | 2.72 | 2.98 | 2.46 |
| 14:00 | 1187 | FC Ingulets vs FC Metalist 1925 | 1.66 | 3.34 | 4.83 |
| 14:00 | 5463 | FK Lviv vs Chernomorets Odessa | 11.29 | 4.93 | 1.22 |
| 14:30 | 1306 | Yunnan Yukun vs Shaoxing Shangyu Pterosaur | 1.43 | 4.05 | 6.44 |
| 15:00 | 3174 | FC Kryvbas Kriviy Rih vs FC Metalist Kharkiv | 1.64 | 3.60 | 4.53 |
| 15:30 | 5646 | Duzyurtspor vs Belediye Vanspor | 2.13 | 2.96 | 3.43 |
| 16:00 | 3058 | Karaman Belediyespor vs Ayvalikgucu | 2.03 | 3.01 | 3.63 |
| 16:00 | 4733 | Lernayin Artsakh vs Ararat Yerevan | 3.95 | 3.10 | 1.77 |
| 17:00 | 2780 | CA Sarmiento de Junin vs Gimnasia de la Plata Reserve | 2.47 | 3.10 | 2.69 |
| 17:00 | 2824 | Argentinos Juniors Reserve vs CA Talleres de Cordoba Reserve | 1.87 | 3.21 | 3.93 |
| 17:00 | 5383 | Rosario Central Reserve vs Banfield Reserve | 1.98 | 3.31 | 3.42 |
| 18:00 | 2116 | Flora II vs FC Elva | 1.64 | 4.46 | 4.25 |
| 18:30 | 3456 | MP Mikkeli vs Kerho 07 | 2.06 | 3.40 | 3.04 |
| 19:00 | 1096 | Jedinstvo BP vs Rudar Pljevlja | 2.30 | 3.17 | 2.85 |
| 19:00 | 2836 | Viimsi JK vs FC Tallinn | 1.71 | 4.28 | 3.96 |
| 19:00 | 3543 | Petrovac vs Iskra | 1.84 | 3.26 | 3.99 |
| 19:00 | 4130 | FA Tartu Kalev vs JK Welco Elekter | 2.15 | 3.50 | 2.55 |
| 19:00 | 4170 | Jezero vs Decic Tuzi | 2.05 | 3.01 | 3.58 |
| 19:00 | 4226 | Mornar Bar vs Buducnost | 3.61 | 3.30 | 1.92 |
| 19:00 | 4247 | FK Arsenal Tivat vs Sutjeska | 6.64 | 3.99 | 1.43 |
| 19:00 | 5351 | FC Nomme United vs Paide Linnameeskond | 1.21 | 7.05 | 10.04 |
| 19:30 | 3405 | Budissa Bautzen vs Oberlausitz Neugersdorf | 1.29 | 5.00 | 6.00 |
| 19:30 | 5670 | Wacker Nordhausen vs FC An Der Fahner Hohe | 1.97 | 3.88 | 3.00 |
| 20:00 | 1118 | Degerfors vs Hammarby | 3.58 | 3.43 | 1.85 |
| 20:00 | 1518 | Erzin Bld vs Ankara Demirspor | 2.05 | 3.05 | 3.52 |
| 20:00 | 1678 | Kasimpasa Erokspor vs Osmanlispor | 1.84 | 3.32 | 3.94 |
| 20:00 | 2076 | SC Gleisdorf vs Pasching | 4.77 | 4.26 | 1.53 |
| 20:00 | 3730 | Orduspor 1967 vs Kusadasispor | 1.80 | 3.15 | 3.70 |
| 20:00 | 5276 | Amedspor vs Anagold 24erzincanspor | 2.22 | 3.01 | 3.16 |
| 20:15 | 4770 | Kray vs TUS 64 Bosinghoven | 4.14 | 4.66 | 1.55 |
| 20:30 | 1653 | Mallorca vs Valencia | 3.14 | 2.89 | 2.35 |
| 20:30 | 3168 | Ankaragucu vs Basaksehir | 2.40 | 3.36 | 2.59 |
| 21:00 | 3146 | Uruguay U20 vs England U20 | 2.69 | 3.11 | 2.46 |
| 21:00 | 3314 | France U20 vs Gambia | 1.38 | 4.34 | 6.82 |
| 21:00 | 3630 | KA Akureyri vs Vikingur Reykjavik | 3.16 | 3.63 | 1.97 |
| 21:30 | 1424 | Servette Geneva vs FC Basel | 1.74 | 3.78 | 4.04 |
| 21:30 | 1606 | FC Winterthur vs FC Zurich | 2.68 | 3.26 | 2.46 |
| 21:30 | 1670 | Grasshoppers vs St. Gallen | 2.62 | 3.67 | 2.32 |
| 21:30 | 1803 | FC Sion vs FC Luzern | 3.10 | 3.47 | 2.11 |
| 21:30 | 2770 | FC Lugano vs BSC Young Boys | 3.32 | 3.58 | 1.98 |
| 21:30 | 3046 | Cosenza vs Brescia | 2.72 | 2.99 | 2.58 |
| 22:00 | 2182 | Manchester Utd vs Chelsea | 1.63 | 3.89 | 4.55 |
| 22:00 | 4088 | Red Star Belgrade vs Cukaricki St | 1.27 | 4.78 | 9.77 |
| 22:15 | 1380 | IH Hafnarfjordur vs Arbaer | 3.20 | 4.40 | 1.67 |
| 22:15 | 1398 | Breidablik vs Valur | 1.99 | 3.78 | 3.00 |
| 22:15 | 2090 | Ellidi vs Kari | 2.64 | 3.83 | 2.17 |
| 22:15 | 3856 | Moreirense vs Covilha | 1.45 | 4.26 | 5.81 |
| 22:30 | 4701 | Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.85 | 3.15 | 2.38 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA YAMPIGIA HESABU GOLIKIPA WA GEITA GOLD

**Na Saada Akida**

GOLIKIPA wa Geita Gold FC, Arakaza Mc Arthur, anatajwa kuwindwa na Simba ambayo inajipanga kuongeza nguvu katika safu hiyo baada ya mlinda mlango wake namba mbili, Beno Kakolanya, kusajiliwa na Singida Big Stars ya mkoani, Singida.

Kakolanya ameshasaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia Singida Big Stars hivyo Wekundu wa Msimbazi inasaka kipa atakayesaidiana na Aishi Manula.

Taarifa za zilizopatikana jijini zinasema Simba imeanza mchakato wa kuzungumza na Arakaza kwa ajili ya kujiunga na klabu hiyo ya Dar es Salaam.

"Sasa hivi tunahitaji kufanya usajili mkubwa na kuangalia kipa ambaye atakuja kuchukuwa nafasi ya Kakolanya na kuleta ushindani na kipa namba moja (Manula)," kilisema chanzo chetu. Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili suala la usajili kuelekea msimu ujao limeongezewa mikakati kwa sababu wanataka kunasa wachezaji wenye viwango vizuri na kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Roberto Oliviera 'Robertinho'.

Ahmed alisema ni mapema kuzungumzia ni mchezaji yupi wanazungumza naye kwa sababu viongozi kwa kushirikiana na kamati ya usajili wanaendelea kufanyia kazi tathmini ya awali ili kufikia malengo ya klabu.

"Kuhusu suala usajili tayari tumeanza mikakati, tunaelewa tumekosea wapi na kitu gani tunapaswa kufanya ili tuwe bora msimu ujao, ni jambo jema kutambua kila hatua ya usajili wa wachezaji ambao tumelenga kuwasajili kupitia viongozi na ripoti itakavyoonyesha mahitaji yetu," alisema Ahmed.

Gazeti hili lilipomtafuta Arakaza, alisema taarifa hizo naye anaziona na kuzisikia mitandaoni kwa sababu hajafuatwa na kiongozi yoyote na bado ana mkataba Geita Gold FC.

"Hakuna mchezaji ambaye hatamani kucheza timu kubwa, nitakuwa tayari kama watakuja na ofa nzuri lakini kwa sasa nawapa kipaumbele Geita Gold FC ambao wameonyesha nia ya kuniongezea mkataba mwingine," alisema Arakaza.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea fulana aliyokabidhiwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Pindi Chana, wakati wa kukabidhi andiko la ombi la Tanzania, Kenya na Uganda kuwa mwenyeji wa Fainali za Kombe la Afrika (AFCON 2027), katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Magoli 15

INATOKA UK. 24

sare nyingine kwa Wanajangwani ni ya 1-1 ugenini dhidi ya Real Bamako ya Mali (ugenini) Februari 26 mwaka huu.

Takwimu hizo zina maana kwamba, Yanga hadi inatinga fainaili, imeruhusu mabao matatu katika mechi 10. Yanatokana na mechi za ushindi wa 3-1 dhidi ya TP Mazembe, sare ya 1-1 dhidi ya Real Bamako na ushindi wa 2-1 katika mechi ya pili ya hatua ya nusu fainali ugenini Afrika Kusini dhidi ya Marumo Gallants.

# Rais Samia abariki AFCON

INATOKA UK. 24

kutaongeza hamasa zaidi kwa ukuaji wa michezo hususan soka.

Alisema aidha michuano hiyo itachangia katika ukuaji wa utalii kwa kuwa ni mashindano ambayo hutazamwa na zaidi ya watu bilioni moja barani Afrika na maeneo mengine duniani kwa ujumla.

Vile vile, Rais Samia amesema mashindano hayo yataleta watu mashuhuri nchini wenye ushawishi duniani hivyo huwezesha na kunufaisha sekta nyingi za uchumi ambapo huchangia ajira, mapato kwa wafanyabiashara na serikali.

Kwa upande mwingine Rais Samia amesema Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imeshafanya utafiti na kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa maandalizi ya kuwa mwenyeji wa mashindano hayo.

Mashindano ya AFCON yataweka rekodi kwa mara ya kwanza kufanyika katika Ukanda wa Afrika Mashariki tangu yalipoanzishwa rasmi mwaka 1957.

Mwaka 2017, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana wa umri chini ya miaka 17 (AFCON U-17).

# Michezo

Alhamisi Mei 25, 2023
Nipashe




## Saka amalizana na Arsenal hadi 2027

UKURASA 21




# MAGOLI 15 YALIVYOANDIKA HISTORIA MPYA YA YANGA SC

**Na Adam Fungamwango**

YANGA imefunga mabao 15 katika mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, huku nyota wake wa kigeni waking'ara kwa kupachika asilimia 87 ya magoli yote.

Yanga ndio wawakilishi pekee wa Tanzania na Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Jumapili watawakaribisha USM Alger kutoka Algeria katika mchezo wa kwanza wa hatua ya fainali utakaoanza saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Chini ya kocha raia wa Tunisia Nasreddine Nabi, Yanga katika mechi hizo 10, imefunga magoli tisa nyumbani, mshambuliaji wake anayewika Afrika kwa sasa Fiston Mayele akitupia mara sita. Yanga imeshinda michezo saba, imetoka sare mara mbili na imepoteza mchezo mmoja.

Straika Mayele, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), anafuatiwa na winga Mzambia Kennedy Musonda aliyejiunga nao dirisha dogo la usajili wa Januari mwaka huu. Ana mabao matatu.

Viungo Mudathir Yahaya na Farid Mussa ni wazawa pekee waliofanikiwa kufunga magoli katika mashindano hayo, kila mmoja ana goli sawa na viungo wageni Tuisila Kisinda, Jesus Moloko, Stephane Aziz Ki na Bernard Morrison.

Wabongo wote walifunga mabao katika mechi mbili dhidi ya TP Mazembe ambazo Yanga ilishinda 3-1 nyumbani na 0-1 ugenini. Mudathir alifunga nyumbani Februari 19 mwaka huu na Farid akafunga goli pekee la mechi ya pili ugenini Lubumbashi Aprili 2 mwaka huu.

Katika mechi zote 10, Yanga haikupata bao katika mechi mbili, lakini ikawa na wastani wa kufunga walau goli moja katika mechi zake. Haikufunga katika kipigo cha 2-0 dhidi ya US Monastir na suluhu ya kwanza nyumbani msimu huu katika mashindano yote, ikilazimishwa na Rivers United ya Nigeria Aprili 30 mwaka huu.

Mbali na mechi hiyo ya Rivers United,

INAENDELEA UK. 23

## Rais Samia abariki kuandaa AFCON

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na Kenya na Uganda kupitia Pamoja Bid wamedhamiria kuwa mwenyeji wa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mwaka 2027 (AFCON 2027), imefahamika rasmi.

Akizungumza jijini, Dodoma jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, alisema nchi hizo zinawania nafasi hiyo kwa kutambua mafanikio makubwa ambayo sekta ya michezo imepata, hivyo kuwa wenyeji wa AFCON

INAENDELEA UK. 23



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea andiko la ombi la Tanzania, Kenya na Uganda kuandaa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027), kutoka kwa Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia, katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >